

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Tano – Tarehe 6 Februari, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kikao chetu cha Tano cha Mkutano wa Sita. Maswali leo tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki. Mheshimiwa Anne Kilango.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 53

Suala la Shughuli za Serikali Kuhamia Dodoma

MHE. ANNE K. MALECELA aliuliza:-

Mara nyingi majibu ya Serikali kuhusu swali la Makao Makuu ya Serikali kuhamia Dodoma yamekuwa 'tumo mbioni' au 'kasungura kadogo' na wakati huo ujenzi wa majengo ya Wizara na nyumba za Serikali unaendelea Dar es Salaam.

Je, Serikali inaweza kuwapa Watanzania ratiba ya uhakika itakayotekelezeka kuliko kuwaweka katika hali ya kutokuelewa hali halisi ya suala hilo muhimu sana na la Kitaifa ?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikijibu swali la Bunge Namba 778 la Mheshimiwa Dokta David Mciwa Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, nilieleza dhamira ya Serikali ya kuhamia Dodoma na umuhimu wa kufanya maandalizi ya msingi ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu na huduma nyingine muhimu zinazohitajika kwa ajili ya kuwaweka watu wa ziada Dodoma na kuendesha shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendeleza zoezi la kujenga miundombinu na huduma nyingine kwa kuzingatia hali ya sasa, Serikali imeamua kuupitia upya mpango kabambe wa Mji Mkuu Dodoma na tayari Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu imepatiwa fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kwa kazi hiyo. Baada ya kukamilika kwa kazi hii, Serikali itaweza kuweka ratiba ya namna ya kutekeleza programu ya kuhamisha Serikali Dodoma, hatua kwa hatua kadri bajeti itakavyoruhusu. *(Makofi)*

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mwaka 1974 wakati Marehemu Baba wa Taifa akiwa ndiye Rais wa nchi hii, kulikuwa na Waziri wa Nchi, Ustawishaji Makao Makuu ya Dodoma, na mimi nakumbuka wakati ule Waziri wa kwanza alikuwa Chifu Adam Sapi Mkwawa, kama kweli Serikali iko *serious* katika kuhamisha Makao Makuu yawe ni Dodoma, kwa nini imemwondoa Waziri wa Nchi yule ambaye alikuwa anasimamia vizuri uhamishaji wa Makao Makuu kuja Dodoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hivi Serikali inaweza ikatuambia kwamba kazi za CDA kwa sasa hivi ni zipi? Kama si wao kugawa viwanja tu na kazi ambayo ingepaswa ifanywe na Halmashauri ya Manispaa ya Jiji la Dodoma? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa swali lako zuri. Ningependa kukumbusha tu pia katika Mawaziri wa Ustawishaji Makao Makuu mmojawapo ambaye amewahi kuwa ni Mheshimiwa Samuel Sitta. Ahsante sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwanza kwa kuona umuhimu mkubwa wa Mji Mkuu wa Taifa letu kuhamia Dodoma na wakati wote Mheshimiwa Anne Malecela amekuwa akisimamia vitu anavyoviamini kwa nguvu zote, kwa hiyo, nampongeza. *(Makofi)*

Ya pili ni kweli kwamba kumeshakuwa na Mawaziri wa Nchi ambao walikuwa na dhamana ya Ustawishaji wa Mji Mkuu Dodoma na ni kweli kwamba sasa hivi hatuna Waziri ambaye jina la Wizara yake ni ya Ustawishaji wa Makao Makuu. Lakini kuna Waziri mwenye dhamana hiyo na Waziri huyo ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye anashughulikia Sera Uratibu na mambo ya Bunge pamoja na siasa. Kwa hiyo, pamoja na kwamba hakuna jina la Wizara kama ilivyokuwa zamani, bado kuna Waziri mwenye dhamana ya kusimamia uhamishaji wa Mji Mkuu kuja Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya CDA siyo tu kupima viwanja. CDA toka wakati huo ambapo kulikuwa na Mawaziri ambao Wizara zao zilikuwa zinaitwa ya Kustawisha Makao Makuu imekuwa ikifanya kazi nyingi na hadi leo inaendelea kufanya kazi nyingi. Kwa mfano, viwanja ni kweli vimepimwa 13,000 kama moja ya kazi ambazo zinapaswa kusimamia. Kwa sababu mji wetu mkuu lazima upangwe vizuri na kama tunataka uwe na mpangilio mzuri basi kazi hii au jukumu hili la kuona kwamba kuna viwanja ni muhimu sana. Lakini ya pili, kuna ujenzi wa awamu ya kwanza wa miundombinu ambazo ni kilomita 30.8 zitakazogharimu jumla ya shilingi bilioni ishirini na mbili, milioni mia mbili ishirini na tisa na zaidi.

Kwa hivyo na awamu ya pili itahusisha kilomita 11.47 za barabara maeneo ya Kizota na majukumu mengine chungu mzima. Vilevile kuna utandazaji wa mabomba ya maji safi yenye urefu wa kilomita tisa kutoka Kilimani hadi Kisasa na vilevile zitagharimu dola za Kimarekani milioni 1,650 na zaidi. Vilevile kuna mradi wa usambazaji wa mabomba ya maji kilomita 21.3 eneo la Kisasa. Pia Serikali imepandisha hadhi ya Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, kazi hiyo yote inafanywa na Mamlaka ya Ustawishaji wa Mji Mkuu.

Kwa hivyo pamoja na kupima viwanja, Mamlaka ya Ustawishaji wa Mji Mkuu Dodoma ina majukumu chungu mzima ya kuhakikisha kwamba Mji wa Dodoma unapangika vizuri, mji wa Dodoma unaendelea na sisi wote ni mashahidi katika muda mfupi Dodoma imekuwa na dalili nzuri. Kwa hiyo, hatuna sababu kwa kweli ya kukataa. Naomba Mheshimiwa Mbunge Anne Kilango Malecela aendeleo kutuhimiza na Serikali itachukua majukumu ipasavyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ujenzi huu wa Makao Makuu Dodoma na kuhamia imechukua muda mrefu sana kiasi ambacho miji au nchi kama Malawi imeweza kuhamia Lilongwe, nchi kama Nigeria imeweza kuhamia Abuja, wakati sisi tulianza mwanzo na sasa hivi kunazungumzwa kujenga mji mpya Kigamboni, je, kwa nini Serikali ina mipango ya kubadilika badilika na kama haikuwa na fedha ya kujenga Makao Makuu Dodoma kwa nini ipate fedha za kujenga Kigamboni sizingehairishwa ikaja kujenga Dodoma? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza inatia moyo sana na inafurahisha Serikali kwamba Wabunge wanataka kuona mji wao mkuu unaendelea na kwamba Makao Makuu ya Serikali yanahamia Dodoma. Mimi nashukuru na nawapongeza Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kila jambo zuri lazima kipewe muda wa kutosha. Tunataka Mji wa Dodoma uwe mji wa kisasa, uwe mji mzuri na Makao Makuu ya Taifa letu na kwa hivyo, suala la muda ni muhimu lakini na mimi nafikiri kwamba tutahimiza ili hatimaye tuhamie kabisa Dodoma.

Lakini suala la Kigamboni ni muhimu vilevile kwa sababu Dar es Salaam itabakia Makao Makuu ya kibiashara na ikiwa ni Makao Makuu ya kibiashara lazima upanuzi wa mji wa Dar es Salaam nao uwe na mpangilio nzuri na moja ya mambo ambayo yatafanya mji upanuke vizuri ni kutayarisha mji mwingine Kigamboni. Kwa hiyo, Serikali itaona kwamba kujengwa Kigamboni hakutapunguza nguvu ya kujenga Dodoma kama Makao Makuu yetu ya Taifa. *(Makofi)*

MHE. FELISTER A. BURA: Kwa kuwa wazo la kujenga na Serikali kuhamia katika Mji wa Dodoma ni zaidi ya umri wa mtu mzima na kwa kuwa tunashuhudia Wizara mbalimbali zikijenga ofisi zao za Makao Makuu Dar es Salaam na ushahidi ni mwaka jana tu Wizara ya Nishati na Madini waliomba fedha kwa ajili ya kujenga Makao Makuu Dar es Salaam, kama Serikali ina nia ya dhati ya kuhamia Dodoma, ninaomba Serikali iseme ni Wizara ngapi tangu wazo la kuhamia Dodoma likubalike na Serikali ni Wizara ngapi zimeshajengwa Dodoma?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, bado azma ya Wabunge ni ile ile ya kuharakisha ukamilishaji wa ujenzi wa Makao Makuu ya Taifa Dodoma. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Felister Bura vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote ni mashahidi kwamba Serikali ilisimamisha ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Nishati na Madini. Hii ni dalili nzuri na kwamba Wizara ya Kilimo imejenga Ofisi yake nzuri hapa. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imejengwa hapa na Wizara zingine zote baada ya mji wa Serikali kukamilika zitaanza kujenga Makao Makuu ya Taifa letu na Makao Makuu ya Wizara zetu mbalimbali na hata hivyo, hata Ikulu yenyewe inajitayarisha kuimarisha Chamwino. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waiamini Serikali yetu na azma yake ya kukamilisha ujenzi wa Mji Mkuu Dodoma. Mimi mwenyewe nitafurahi sana kwa sababu Hanang ni hapo karibu, makao makuu yakiwa hapa itakuwa ni faraja kubwa na itakuwa ni mwendo mfupi tu kuja makao makuu na wewe Naibu Spika nina hakika utafurahi. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na tunashukuru sana. Tuendeleo bado tuko Dodoma, Mheshimiwa Dokta David Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini.

Na. 54

Fidia kwa Wananchi Waliohamishwa Eneo la Nzuguni Kwenye Machimbo ya Dhahabu

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE aliuliza:-

Wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu eneo la Nzuguni walisimamishwa na kuondolewa ili kupisha eneo la jeshi.

Je, Serikali iko tayari kuwalipa wananchi hao fidia zao mapema iwezekanavyo kama ilivyowaahidi wananchi hao ili kuepusha usumbufu wa ufuatiliaji wa kila siku?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta David Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika mwaka 1994 wachimbaji wadogo wadogo walikuwa wakichimba dhahabu katika eneo la Nzuguni. Wachimbaji hao waliondolewa ili kupisha eneo hilo kuchukuliwa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali imekamilisha taratibu za kuwatambua wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu wale 39 wa eneo hilo la Nzuguni wanaostahili kulipwa fidia yao mali zao pamoja na maendeleo yaliyokwishafanyika vimethaminiwa na thamani yake ni shilingi 195,909,000/=. Nyaraka zote zinazohitajika kwa ajili ya kufanya malipo zimekamilika na kukabidhiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo ndiyo yenye jukumu la kufanya malipo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani tayari ilikwishaweka katika mpango na bajeti yake ya mwaka huu (2011/2012) lakini kutokana na ufinyu wa bajeti wachimbaji hao watalipwa fidia zao katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelezo haya, ni dhahiri kwamba Serikali ina dhamira ya dhati ya kuwalipa fidia wachimbaji hawa wadogo wadogo wa dhahabu eneo la Nzuguni na hivyo kumaliza kero yote. *(Makofi)*

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kushukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri. Nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa kazi mojawapo ya Serikali yetu nzuri ya Chama cha Mapinduzi ni pamoja na kuwaondolea wananchi kero zote zinazowakabili katika maisha yao ya kila siku. Je, Serikali yetu ina mpango mkakati upi wa kuweza kulipa fidia zote za wakazi wa Mji wa Dodoma hasa zile zinazohusiana na mashamba pamoja na nyumba zilizobomolewa na CDA ili kuwaondolewa wananchi wetu usumbufu wa kufuatilia madai yao kila siku?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Serikali imetoa jibu la msingi kwa hawa wachimbaji wadogo wadogo. Maelezo haya pia yanajikita kwenye shughuli zote za ulipaji fidia kwenye maeneo yote yanayotakiwa na Serikali ambayo yalikuwa yanamilikiwa na wananchi kwenye maeneo husika.

Katika Halmashauri ipo timu ambayo inafanya kazi ya uthamini pale ambapo Serikali inahitaji eneo hilo kulifanyia kazi. Pale tuna Afisa Ardhi na tuna Afisa Mthamini lakini pia Mamlaka zinazohusika akiwemo Mkuu wa Wilaya nao pia ni miongoni mwa timu ambayo inatakiwa kufanya kazi hiyo ya uthamini pindi inapohitaji eneo hilo kulifanyia kazi kwa Serikali. Kwa hiyo, jitihada za Serikali kulipa malipo ya fidia ya maeneo yote yanayohitajika kwa shughuli maalum zinafanywa katika kila eneo. Tunachofanya sasa ni kuhakikisha tu kwamba fedha zinatengwa kwa ajili ya bajeti hiyo. Inawezekana pia hata kabla ya maamuzi ya kuchukua eneo hilo haijakamilika na fedha yao iwe imeshatengwa tayari.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Suala la Mheshimiwa Dokta Mallole linafanana kidogo na hali ilivyo katika jimbo langu la Singida Mashariki ambako katika eneo la Taru, kijiji cha Sambaru mwaka jana kati ya Oktoba na Novemba wananchi zaidi ya 3,000 walitimuliwa katika maeneo yao, walitimuliwa katika makazi yao kwa amri ya Mkuu wa Wilaya ili kupisha mgodi wa dhahabu na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alishaliambia Bunge hili kwamba kampuni ya *Shanta Mining* haina leseni ya kuchimba dhahabu eneo la Taru.

Sasa naomba nijibiwe kwa nini wananchi wanafukuzwa katika maeneo yao ili ipewe kampuni ambayo haina leseni ya kuchimba madini? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Kwa kuwa swali hili ni mahususi, sina hakika kama..., Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana pia kweli kama Waziri wa Maliasili analitambua jambo hili na alishawahi kutoa tamko hapa na kwamba ameahidi kwamba utekelezaji wa jambo hilo unaweza

kufanywa, linaweza kufanywa kwa sababu Serikali kama ambavyo nimesema kwenye jibu la msingi kwamba Serikali inapohitaji kufanya mabadiliko ya matumizi ya ardhi au eneo lolote lile lazima Serikali iwe imeshajipanga kuweza kuandaa utaratibu wa bajeti yake pindi watakapotoa agizo la kuwaondoa. Kama jambo hilo sasa limefanyika tutawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini tuone hali hii ikoje na baadaye tutakupa mrejesho Mheshimiwa. Ahsante sana.

Na. 55

Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Bweni Kata ya Vigwaza

MHE. ZAYNAB M. VULLU aliuliza:-

Kutokana na juhudi kubwa ya wananchi wa Vigwaza, Jeshi la Wananchi (JWTZ) liliridhia kuwakabidhi wananchi eneo na majengo yaliyoko kijiji cha Milo Kata ya Vigwaza – Bagamoyo yaliyokuwa yanatumiwa na wapigania uhuru wa Chama cha P.A.C cha Afrika Kusini kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha majengo hayo ili kuanzisha shule ya bweni ya Kata ya Vigwaza?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Kata ya Vigwaza kwa jitihada walizoonessa katika kuhitaji shule kwa ajili ya kidato cha tano na sita ili kuwapatia fursa watoto wanaohitimu na kufaulu vizuri masomo yao ya kidato cha nne ili kuendelea na kidato cha tano. *(Makofi)*

Napenda kutumia nafasi hii pia kulishukuru Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kwa kuridhia kukabidhi eneo hilo na majengo yake kwa wananchi wa Kata ya Vigwaza ambalo eneo lilikuwa la wapigania Uhuru wa Chama cha PAC cha Afrika Kusini, kwa wananchi wa Kata ya Vigwaza. Jeshi la Wananchi Tanzania liliridhia na kukabidhi kambi iliyokuwa inatumiwa na wapigania Uhuru wa iliyoko kijiji cha Milo katika Kata ya Vigwaza kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo tarehe 13 Oktoba, 2009 na hati rasmi ya makabidhiano ya eneo hilo *(DET Masuguru)* ilishakabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya tarehe 2 Novemba, 2009. Na ukubwa wa eneo lililokabidhiwa ni ekari 4,000 sawa na hekta 1,600 ambalo linatosha kabisa kutumika kwa shughuli za kielimu na jumla ya wanafunzi 960 wanaweza kunufaika kwa kuwa katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya majengo yaliyakabidhiwa ni kama ifuatavyo; Jeshi la Wananchi limekabidhi nyumba tano ambazo zinaweza kutumika kama nyumba za walimu, bwalo moja ambalo linaweza kutumika kama maabara, ghala moja la vifaa ambalo linaweza kutumika kama bwalo na zahanati moja. Aidha, majengo mengine yaliyopo yanahitaji ukarabati ili kupata nyumba na madarasa pamoja na vyoo. *(Makofi)*

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu Serikali Kuu inaahidi kutoa kiasi gani au mchango gani ili kuweza kufanikisha ujenzi huo ambao Halmashauri zetu sote tunafahamu kiwango chake cha pesa ni kidogo sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, ni lini ujenzi huo unatarajiwa kukamilika ili vijana wetu waweze kupata elimu ya kidato cha tano na sita katika shule hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vullu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ambalo lilikuwa linatumwa na Jeshi la Wananchi ambalo wamelikabidhi pia kwa Halmashauri ya Wilaya, maamuzi ya uendelezaji wa eneo hili yanafanywa na mamlaka iliyokabidhiwa baada ya kuona changamoto na kipaumbele kwenye maeneo yao. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imeona eneo hili litumike kama sekondari na kutokana na mahitaji ya eneo hilo lilipo kwa mfano, Diwani na Kamati yake ya Maendeleo kwenye eneo lile ndio ambao waliona kwamba majengo haya baada ya wale kuondoka na kukabidhiwa yana umuhimu wa kuanzisha shule ya sekondari ya kidato cha tano na cha sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maamuzi hayo sasa Baraza la Madiwani la Halmashauri husika litapanga bajeti yake kwa ajili ya kuendeleza hicho ambacho wameamua. Kwa Vigwaza, wameamua iwe ni kidato cha tano na sita ; lakini pia, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imeshapanga kufanya ukarabati wa majengo yale na maeneo hayo, wameamua pia waongeze madarasa kumi pamoja na hosteli mbili. Kwa hiyo, mpango wa kuendeleza eneo hilo upo tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie nafasi hii, Mheshimiwa Mbunge najua uwezo wako, utakapopata nafasi ya kutembelea Bagamoyo au kwenye Wilaya zako ikiwemo Bagamoyo, pita pale, ongeza hamasa ili Halmashauri ziweze kutenga bajeti zao kwa ajili ya kuboresha eneo hilo ili azma iliyokusudiwa iweze kutimia. Serikali Kuu kwa maana ya Halmashauri kwa maana ya TAMISEMI, kupitia mipango yake na bajeti ambazo tunapeleka katika Halmashauri kila wakati, basi pindi watakapopata fedha yao wanaweza kutenga tena kuongeza nguvu, uanzishaji wa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kuanza kwa ujenzi huu ni pale ambapo Halmashauri yenyewe imepanga ujenzi huo uanze lini na utakamilika lini. Lakini sisi tunawasisitiza kukamilisha taratibu hizo mapema ili vijana waweze kunufaika na eneo hilo.

56

Mradi wa Mabasi ya Wanafunzi

MHE. PHILIPA G. MTURANO aliluliza:-

Kutokana na kuongezeka kwa wanafunzi katika mikoa mbalimbali hususan kwa shule zilizo mijini hapa nchini, kumesababisha kuwepo kwa usumbufu mkubwa sana kwa wanafunzi kwenda na kurudi shuleni:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua mradi wa usafiri wa mabasi ya wanafunzi?

(b) Je, kwa nini Serikali isiwape vibali wafanyabiashara wenye mabasi watoe huduma hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philipa Geoffrey Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo kwamba, Serikali inalitambua tatizo la wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wanaotumia usafiri wa mabasi kwenda shuleni na kurudi nyumbani baada ya masomo hasa maeneo ya mijini. Changamoto hii kutokana na ukweli kuwa mabasi ya wamiliki binafsi huwajali zaidi abiria wa kawaida ambao hulipa nauli kubwa na hivyo kuwaacha wanafunzi walio wengi katika vituo vya mabasi asubuhi na kusababisha kuchelewa masomo shuleni. Hali huwa hivyo wakati wa kurudi nyumbani baada ya masomo kwa kuachwa vituoni na kuwasababishia pia kuchelewa kurudi nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kujibu swali (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hivi sasa inashirikiana na sekta binafsi katika kutoa huduma ya usafiri wa mabasi kwa wanafunzi na wananchi kiujumla. Hii inatokana na sera ya Serikali kujitoa katika

kufanya biashara na hivyo kuachia sekta binafsi kuendesha huduma hiyo. Jukumu la Serikali kwa sasa ni kupanga na kusimamia viwango vya nauli. Aidha, katika maeneo mbalimbali nchini Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikishirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kutoa huduma hiyo. Mfano katika Jiji la Dar es Salaam, Jiji kama Tanga, Mwanza, Mbeya na hata hapa Dodoma. Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) lilipokea jumla ya mabasi matano yaliyotolewa na Benki ya CRDB ili kuendelea kutoa huduma ya kubeba wanafunzi jijini. Mabasi hayo husafirisha wanafunzi tu na kufanya kazi kwa saa mbili asubuhi na saa mbili jioni ili kuwapeleka na kuwarudisha wanafunzi na nauli wanayolipa bado ni shilingi 150/= tu. Hayo ndiyo makubaliano kati ya CRDB na UDA. Pamoja na kuwepo kwa mabasi hayo, bado matatizo ya usafiri wa wanafunzi jijini yapo kwa sababu ya uchache wa mabasi hayo ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi waliopo Jijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa fursa kwa wafanyabiashara wenye uwezo wa kusafirisha abiria wakiwemo wanafunzi, kutoa huduma hiyo kwa kupeleka maombi yao katika mamlaka zinazohusika na utoaji wa leseni za usafirishaji wa abiria. Lakini napenda nitumie nafasi hii pia kuwakumbusha Watanzania wote kwamba jambo hili ni letu sote na kweli ni lazima tujitokeze katika kuwasaidia watoto wetu kwenda shuleni kwa wakati na kurudi kwa wakati. Nitumie pia fursa hii kuwashauri Waheshimiwa Wabunge, kuwahamasisha wafanyabiashara waliopo katika maeneo yetu ambao wapo tayari kutoa huduma hii ya kusafirisha wanafunzi hawa ili waweze kuwahi kwenda masomoni na kurudi majumbani mwao. *(Makofi)*

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi na hili jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu haya mabasi yaliyotolewa na CRDB kusaidia usafiri wa wanafunzi Mkoa wa Dar es Salaam, binafsi sijaona hilo. Wanafunzi pale wameendelea kupata matatizo sana na Mkoa wa Dar es Salaam ambao ameutolea mfano Mheshimiwa Waziri, ulikuwa na mradi wake wa mabasi ya kutosha kabisa kuwapeleka wanafunzi shuleni; mradi huo haujulikani uko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali; hawa watu ambao waliuhujumu mradi huu, Serikali imewachukulia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, lengo la mfanyabiashara yeyote yule ni kupata faida. Sasa Serikali pamoja na kutoa wito kwamba Waheshimiwa Wabunge waweze kufanya mipango labda kuongea na watu wanaomiliki mabasi binafsi ili waweze kusaidia kutoa huduma ya mabasi kwa wanafunzi. Je, Serikali inatengeneza mazingira gani ya kuwashawishi wafanyabiashara ili waweze kukubali kuwasafirisha hawa wanafunzi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mturano, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba mabasi yaliyotolewa na CRDB kwa UDA yapo na yanafanya kazi na yapo sana kwenye route ya Gongo la Mboto kwenda katikati ya Jiji, Mbagala kwenda katikati ya Jiji, lakini lipo basi linatoka Kimara kwenda katikati ya Jiji. Lakini lipo basi moja linaanzia Kongowe kwenda Kivukoni; hayo ni baadhi ya mabasi ambayo hata mimi nimeshuhudia kuyaona yakitoa hizo huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna suala la waliohujumu mradi huu wa uendeshaji wa mabasi haya. Tatizo la UDA, ninyi wote ni mashahidi limeshawahi kujitokeza na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa agizo kwa CAG kwenda kuikagua UDA na itoe taarifa kwake; kazi hiyo inafanyika na pindi majibu yatakapopatikana kutoka kwa CAG, nadhani tutapata taarifa ili tuweze kujua hatua ambazo zimechukuliwa kwa hawa ambao wamehujumu mradi huu ili pia uendelee kuratibu shughuli zetu kusaidia watoto hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali imeandaa utaratibu mzuri sana wa kupunguza tatizo kubwa la kuondoa usumbufu wa vijana hawa kwenda shule na kurudi kwa mpango wa uanzishaji wa

mabasi yaendayo haraka ambayo tayari ujenzi umeshaanza, wale wachache ambao mmepata nafasi ya kupita kule feri tayari kituo kimeshajengwa, lakini pia tumeona hata hapa Shekilango, kuna kituo kinaendelea kujengwa pale, maeneo ya Mwenge kinajengwa, ile ni jitihada za mradi wa mabasi yaendayo kasi ambao pia utasaidia sana kupunguza msongamano wa wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hili nirudie tena kwa Watanzania wote; ingawa tunajua kwamba mfanyabiashara yoyote yule hufanya biashara kwa ajili ya kupata faida, lakini jukumu la kumlea mtoto huyu na kumsaidia ni letu sote. Naomba sana niwasihi wale wote wenye makampuni ya usafirishaji, wapunguze masharti kwa madereva wao na wapiga debe wao ili madereva hao na wapiga debe hao wanapowakuta wanafunzi waweze kuwabeba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mbunge wa Gairo, Mheshimiwa Shabiby na Mbunge wa Morogoro Mheshimiwa Abood. Mimi mwenyewe nimeona basi la Shabiby likibeba watoto pale Ubena Zomzi likiwapeleka uelekeo wa Chalinze. Hayo ni masharti yake nafuu ambayo madereva wake wameona wanafunzi, wametambua kwamba ni muhimu na wamewabeba.

Naomba sana wafanyabiashara wengine wafuate mwendo huu ili pia tuweze kuwasaidia watoto hawa ili tuondokane na tatizo hili nchini. Tukifanya hilo inawezekana, ahsante. *(Makofi)*

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wabunge tumeshawahamasisha wafanyabiashara wengi sana kusaidia usafiri wa wanafunzi na wengi wamejitokeza. Lakini mamlaka zilizokuwepo ndizo zinawakatisha tamaa wafanyabisahara hawa kwa kuwawekea vikwazo vikubwa sana na kushindwa kutimiza wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi hasa wasichana wadogo, wanaondoka nyumbani saa kumi za usiku/alfajiri na wanarudi saa nne za usiku kutokana na matatizo ya usafiri. Je, Serikali sasa itadhibiti na kuweka sawa mamlaka zake husika zinazowakatisha tamaa na zinazowawekea vikwazo vikubwa sana wafanyabiashara hawa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ambazo zimepewa kazi ya kuratibu shughuli zote hizi zinazo sheria zao na namna ambavyo wanaweza kuziendesha na hawa wamiliki wa mabasi wanapokwenda kukata leseni hupewa masharti hayo.

Pamoja na masharti yale, bado tunaendelea kuwasihi wafanyabiashara hawa kutambua tatizo la watoto wetu kwenye Jiji hili kwamba watoto wetu wanachelewa sana kwenda shuleni na kurudi. Kama ambavyo nimeshauri kwamba wafanyabisahara hawa wakipunguza masharti kwa wafanyakazi wao, madereva na wapiga debe wao, wanaweza pia wakawasaidia kwa kiasi kikubwa vijana hawa kwenda shuleni na kurudi kwa kutumia mabasi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama ambavyo nimeeleza mkakati wa Serikali ambao pia utasaidia jambo hili, uanzishaji wa usafiri wa haraka, hilo pia linaweza kuwa ni njia nzuri ambayo pia itapunguza msongamano wa vijana hao kukosa kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu, alielezea suala la ombi la Waziri Mkuu kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua suala zima la ubinafsishaji wa UDA. Na nadhani Serikali inafahamu kwamba Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma ambayo Kikanuni inashughulikia masuala ya ubinafsishaji, inasubiri sana ripoti ya Mkaguzi Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili Kamati yake Ndogo iweze kufanya kazi yake ya Kikanuni ya kuangalia zoezi zima la ubinafsishaji wa UDA lilivyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inalieleza Bunge hili Tukufu kwamba ni lini ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itakabidhiwa kwa ajili ya Kamati ya Bunge iweze kufanya kazi yake kwa mujibu wa Kanuni?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ameagiza agizo hili na lengo ni kupata taarifa za haraka sana baada ya kazi hiyo ya ukaguzi ili sasa Kamati zote, ile ya Bunge ambayo inafanya kazi ya ufuatiliaji wa uendeshaji wa mashirika haya iweze kupata majibu kwa haraka lakini pia Kamati nayo iweze kutoa taarifa kwa Watanzania juu ya hatima ya ukaguzi ambao unaendelea.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba kadiri ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameagiza kwa haraka, tutapata majibu hayo kwa haraka na nikuahidi kwamba kwa kuwa tayari Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaagiza, sisi tuko tayari sasa kufuatilia kuona kwamba tunapata majibu haya kwa haraka vilevile ili Kamati yako iweze kufanya kazi yake vizuri. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 57

Magonjwa Yanayoshambulia Zao la Ndizi Bukoba

MHE. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza:-

Ndizi ambazo ndio zao kuu la chakula na biashara Bukoba na ambalo hutegemewa na watu wengi, limeshambuliwa na magonjwa mengi kama vile panama, njano, mnyauko, madoa na kadhalika; mazao madogo kama mihogo yameshambuliwa na magonjwa kama batobato na kadhalika:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na magonjwa haya?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi chakula cha dharura hasa wakati huu ambapo magonjwa hayo yameenea na hayajapatiwa tiba?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 1997 Mkoa wa Kagera na nchi jirani zinazopakana na mkoa huo zilikumbwa na magonjwa yanayoshambulia migomba, kahawa, mihogo na viazi vitamu. Ili kukabiliana na kuenea kwa magonjwa hayo, Wizara yangu imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kufanya ukaguzi wa mazao, mbegu na vipando vinavyoingizwa nchini kupitia katika mipaka, bandari na viwanja vya ndege ili kuhakikisha kwamba havina magonjwa na wadudu.

(ii) Kituo cha Utafiti wa Kilimo Maruku, kinazalisha mbegu bora mama za migomba na hutoa miche 34,000 kwa mwaka.

Pia kituo hicho kinatoa mafunzo kwa wakulima jinsi ya kuanzisha vitalu vya migomba isiyo na magonjwa katika vijiji 15 katika Wilaya ya Bukoba.

(iii) Vituo vya Utafiti vya Ukiriguru na Maruku, vimetoa mbegu bora nane za muhogo ambazo hazishambuliwi na ugonjwa. Mbegu hizi ni Mkombozi, Meremeta, Kyaka, Isanzu, Rangimbili, Nyakafuro, Belinde na Suma.

Aidha, mbegu zenye ukinzani na ugonjwa wa batobato kali ya mihogo zimesambazwa katika Wilaya zote za mkoa wa Kagera zinazolima zao la muhogo.

Katika mwaka 2010/2011, Kituo cha Utafiti cha Maruku kimesambaza jumla ya pingili 400,000 za mbegu bora za muhogo zenye ukinzani dhidi ya batobato kali ya muhogo ambazo zimepandwa katika ekari 100 katika Wilaya za Bukoba, Misenyi, Muleba na Biharamulo. (Makofi)

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama chakula cha dharura kinahitajika, uongozi wa Wilaya ya Bukoba unashauriwa kuwasiliana mapema na Wizara yangu na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kitengo cha Maafa) ili tathmini ya msaada ifanyike haraka. (Makofi)

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tumefikia wapi haswa kuhusu tiba ya ugonjwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana amezungumzia hatua inayochukuliwa, lakini sikusikia jibu kuhusu tiba hasa ya ugonjwa wa mnyauko wa migomba. Maana hata hii inayotolewa pale Maruku Kituo cha Utafiti, ikishaenda kwa wakulima kule ikapandwa, baadaye inashambuliwa na ugonjwa huu na inanyauka na inaharibika. Sasa kama kuna tiba yoyote ambayo imepatikana, basi tupate taarifa hiyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa 12 mwaka jana mimi pamoja na Mheshimiwa Anna Tibaijuka, Mbunge wa Muleba Kusini na Waziri wa Ardhini na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Kanali Mstaafu Fabian Massawe, tulitembelea Uganda kwa mualiko wa Rais Museveni, tukaona jinsi ambavyo kule Uganda wanakabiliana na ugonjwa huu wa mnyauko wa migomba. Bado hakuna tiba, lakini wana udhibiti, wana utaalumu ambao wanautumia wakulima wa kule na hawana shida hii ya mnyauko.

Sasa swali, nauliza kama Serikali itakuwa tayari kugharamia wananchi kidogo kutoka Bukoba waende Uganda kule waone jinsi wenzao wanavyofanya kuondokana na ugonjwa huu?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu tiba namba moja na mimi nimeembelea baadhi ya mashamba hayo, ya kwanza kabisa ni kuharibu ile migomba pamoja na wadudu, yote ile ambayo haifai, lakini kubwa zaidi ni hili alilolisema kuhusu tiba ya kudumu. Nakubaliana na ushauri wake aliutoa na ndiyo maana tuna vitengo hivi vya *research* katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ambavyo kazi yao kubwa ni kutazama wadugu gani, magonjwa gani yanaweza kuingia katika nchi na tunayadhibiti namna gani. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba iko haja pia ya kuendelea kutafuta wenzetu wanafanya nini kule na nitawasiliana na kitengo kinachoshughulika na mambo haya kuchukua ushauri ambao ameutoa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba pia niseme kwamba mbali ya magonjwa haya si kwamba tukiweka tiba, basi magonjwa hayawezi kuendelea kuja, ndiyo maana tumejitahidi kuweka vituo mbalimbali katika maeneo ya mipaka yetu takriban mipakani huko. Katika mipaka kama 51 tumeweka vituo vya kukagua vinavyoingizwa na mazao yanayoingizwa ili yasilete magonjwa haya na wadudu hawa, tumeweka kwa sababu hii. Pia nakubaliana naye kwamba, ni kweli tunahitaji kuendelea kufanya uchunguzi wa tiba wa magonjwa haya.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuwa jukumu la kuangalia magonjwa ya mazao ni pamoja na kuangalia magonjwa ya mazao ya pamba na kwa kuwa Serikali ilitoa bilioni nane kwa ajili ya madawa ya pamba na wananchi wamechangia shilingi 15 kwa kilo kwa ajili ya dawa hizo, kina sasa kumetokea ubaguzi, wale wanaolima katika vikundi wanapewa viua vidudu vingi zaidi na wale ambao hawamo kwenye vikundi badala ya kupewa sita wanapewa nne, halafu watu wengine wanaandikishwa ambao ni feki wala siyo wakulima. Jambo hili litapelekea tusiwe na pamba ya kutosha. Je, Serikali inatamka nini juu ya kusema kwamba pembejeo ni kwa ajili ya wakulima wote kwa sababu ni pesa ya umma na lini itaweza kufanya ukaguzi wa Bodi ya Pamba pamoja na CDTF kuhakikisha kwamba fedha za Serikali na za wananchi zinatumiwa sawasawa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza labda nimsahihishe kidogo tu nadhani haviitwi viua wadudu vinaitwa viuatilifu kwa Kiswahili sanifu. Lakini

analosema Mheshimiwa Cheyo ni sahihi, niseme tu kwamba, mara nyingi unakuta namna ya kuwafikia wakulima wengi, inakuwa rahisi kuwafikia wanapokuwa katika vikundi kuliko wanapokuwa mmoja mmoja, lakini haina maana kwamba tunataka tuwabague wakulima hawa. Nadhani tunachoweza sasa kufanya nakubaliana na hoja yake kwamba ni juu yetu sasa sisi na Bodi ya Pamba na wadau wote kuangalia njia bora zaidi itakayowafikia wakulima wote wa pamba. Maana mwisho wa siku hata vile vikundi ni mkulima mmoja mmoja anayeviunda. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Cheyo kwamba lazima tuangalie jinsi gani tutakavyoweza kuwafikia wakulima hao. Lakini kwa sasa tunakwenda kwa vikundi kwa sababu inakuwa ni njia rahisi kabisa kuwafikia wakulima kabla ya kuanza na mmoja mmoja.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya maswali ya msingi, lakini naomba tu nimweleze jambo moja ambalo linatatiza watu wa Kagera. Sisi Wahaya, hatuli ndizi zote hizo ulizotaja, pia na hizo zingine tunazila kama shida au kama kiama kwamba hakuna chakula. Tungeomba tu Serikali ikazanie kabisa kuona ndizi kama Ntobe, Nyoya na zingine zinapata tiba ili tuweze kupata chakula cha kweli bila kuishi kama wakimbizi. Kwa kweli hizo ndizi zingine tunakula kama wakimbizi siyo chakula chetu.

Pili, Serikali ina mpango gani, kuna wadudu wameshambulia vyakula kama mihogo, ndizi migomba na kadhalika. Je, mna utaratibu gani wa kulinda mazao mengine kama maharage kabla hayajashambuliwa?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hawa watani zangu hawapendi kula ndizi zingine amesema ntobe, zingine ziko chakara na zingine nazijua, lakini hizi ndizi ambazo sasa tunazileta ambazo zinaonesha kama ni mazao mapya kidogo kule, kwanza ukizitazama kwanza zina ukinzani na magonjwa ninayoyataja haziharibiki kwa haraka. Lakini pia hizi ndizi zinaweza zikatumika kama biashara maana yake hatulimi tu kwa ajili ya kula, tunalima pia kwa ajili ya biashara. Wengi wamelima ndizi za namna hii na wanazisafirisha kwenda mpaka nje.

Jambo la pili ambalo ningependa nimshauri Mheshimiwa Mshama ni kwamba, hata kula nako au *eating habits* lazima tuzibadili, haiwezekani tukasema lazima tule inshakara, intobe, nanyumu tuliyozoea tu lazima tuwe tunaangalia na vingine vinavyokuja. Kwa hiyo, tufanye yote mawili; *eating habits* tuzibadilishe lakini pia mazao haya ambayo yanaweza kutupatia fedha nyingi za kigeni nayo ni muhimu tuyawekee umuhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazao labda kwa haraka niseme jinsi tunavyoshughulikia mazao mengine, Mabwana Shamba wetu wapo katika vijiji, vile wewe unapoonza matatizo kwenye mazao kama hayo maharage sijui mahindi, muone bwana shamba ili aweze kukushauri kwamba utumie njia gani ya kutibu matatizo hayo. Kama ni mambo makubwa basi wanaleta angalau Wizarani ili tuweze kuyashughulikia kwa ngazi kubwa zaidi.

Na. 58

Kuboresha Bei ya Mazao ya Choroko, Mbaazi na Kunde Nchini

MHE. JEROME D. BWANAUSI aliuliza:-

(a) Kwa kuzingatia kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, ni lini Serikali itaandaa mazingira mazuri kwa wakulima kupata bei nzuri ya mazao ya choroko, mbaazi na kunde kwa mwaka 2012?

(b) Je, lini Bodi ya Mazao Mchanganyiko itashirikiana na Vyama vya Ushirika ili mazao ya choroko, kunde na mbaazi yaingizwe kwenye mpango wa stakabadhi ghalani katika msimu wa 2012?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakulima wa mazao ya jamii ya mikunde zikiwemo choroko na mbaazi kwa muda mrefu walikuwa wakitegemea bei nzuri, waliokuwa wakitegemea soko lisilo na uhakika, jambo ambalo linasababisha wakulima wasipate bei nzuri. Kwa kutambua hilo, Serikali imeanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo itasimamia ununuzi wa mazao ya aina ya nafaka na mengine yasiyo na chombo maalum cha kuyasimamia kama ilivyo kwa mazao kama kahawa, korosho, pamba, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko itashirikiana na Mabara ya Kanda ya Mazao, Vyama vya Ushirika na Wadau wengine ili kuweka mfumo mzuri wa kununua mazao. Mabaraza ya Kanda za Mazao, pamoja na kazi nyingine yataandaa mikakati ya uendelezaji wa mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko, kushirikiana na wadau kutafuta masoko na kupanga bei elekezi katika kila Kanda ya Mazao.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko hivi sasa inaendelea kujenga uwezo wa rasilimali watu, kutayarisha maghala na kuandaa bajeti ili ianze kununua mazao katika msimu wa 2012/2013.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na pia nimshukuru katika jibu lake la msingi amegusia pia suala la korosho, lakini nina maswali mawili kama ifuatavyo: Kwanza, kwa kuwa tangu msimu wa mauzo ya mazao ya korosho uanze tarehe 15 Oktoba, mwaka jana, hali ya soko la korosho imeyumba kiasi cha kuwafanya wananchi wa mikoa yote ikiwemo wale wa Jimbo la Lulindi kukosa fedha pamoja na kutii agizo la Serikali kwamba korosho zote zipelekwe kwenye Vyama vya Ushirika. Je, Serikali inatoa tamko gani leo, kwa wakulima wa korosho ambao sasa takriban miezi sita hawajapata fedha? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Serikali inatambua kwamba suluhisho la tatizo la soko la korosho ni kubangua korosho hizi hapa nchini. Je, Serikali imeweka mkakati gani kuhakikisha kwamba korosho zote zinaweza kubanguliwa hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza juzi tu tarehe mbili tulikuwa na kikao cha wadau wa korosho hapa hapa Dodoma ambacho Waziri alikiitisha na wadau wa korosho walizungumzia mustakabali wa zao hili ikiwa ni pamoja na suala la soko lenyewe. Labda pengine nirudie yale ambayo tayari yameshachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mlikuwa mnafuatilia, Mheshimiwa Waziri ameshatoa siku 16 tu kuanzia siku ile ili hawa wanunuzi wa korosho hasa hasa wale ambao ni wakubwa wanaofanya *curtail* na kusababisha korosho ile iuzwe kwa bei aidha ya kurushwa au isiuzwe wawe wamenunua korosho hiyo katika muda huu na kwamba wasiponunua basi katika siku hizo leseni zao zitasimamishwa. Pia alisema kwamba, siyo leseni zao tu za kununua korosho hata leseni zao za biashara nyingine wanazozifanya hapa nchini, kama wao hawataki kutusaidia katika sekta hii hata leseni zingine pia tutazisimamisha. Hii yote ni kuchukua hatua ili hawa wanunuzi waweze kununua korosho. Jana nimepata taarifa kwamba wameanza kununua, lakini hata hivyo ni kwa kusuasua, bado siridhiki na ununuzi unaofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ningeseema tu kwamba, baada ya Serikali kutoa maelekezo hayo na kama wanunuzi wa korosho wataendelea kufanya fanya *curtail* hizi Serikali haiwezi kufumba macho na kukaa kutazama korosho ikiwaozea wakulima wake. Serikali itakaa pamoja na wadau wote kwa maana ndani ya Serikali yenyewe tunayo Wizara, Hazina, Ofisi ya Waziri Mkuu tutakaa kutafuta ni hatua gani sasa zichukuliwe ili kuokoa zao hili la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haiwezi kushindwa, itatafuta njia, ikiwa ni sambamba na kuwachukulia hatua hao ambao watakuwa wamekiuka. Lakini Serikali itakaa kutafuta njia muafaka ikayofanya sasa korosho za wananchi zinunuliwe. Naomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wanaotoka katika mikoa hii ya korosho, basi tuwe na subira katika huu muda, halafu tutaona Serikali inachukua hatua gani.

Mheshimiwa Spika, na kuhusu kubangua korosho nadhani hili tumelisemea mara nyingi kwamba tungependa tuongeze thamani korosho zibanguliwe nchini ili ziuzwe zikiwa na thamani kubwa. Ndiyo

maana sasa baadhi ya wawekezaji wameanza kuweka viwanda vidogo vidogo vya kubagua korosho. Lakini hata Sheria yetu yenyewe ya Korosho inatuelekeza hivyo na tumeweka makusudi kwamba tutoze ushuru mkubwa kwenye korosho ghafi inayokwenda nje, hiyo ni hatua ya kuwazuia wale wanaopenda kununua korosho ghafi kuipeleka nje, lengo ni kwamba korosho hiyo ibanguliwe hapa nchini.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niliulize swali, kwa kuwa bei nzuri ya mazao inaweza ikawepo tu kunapokuwa na soko la uhakika la mazao hasa ya mchanganyiko na hususan niseme zao la mahindi. Kwa kuwa Serikali mpaka sasa ninavyosema haijaanza kununua mazao kwa maana ya mahindi ya msimu uliopita kwa wananchi wa Wilaya ya Mbozi na maeneo mengi pia hapa nchini ya Mkoa wa Iringa, Ruvuma na huko Rukwa, ni lini sasa Serikali itaanza kununua mahindi katika maeneo yale ambayo mahindi hayajanunuliwa kabisa hasa Wilaya ya Mbozi? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba, kweli ununuzi wa mahindi haujakwenda kama tulivyotarajia. Lengo la *NFRA* ilikuwa kununua tani 200,000 kutoka kwa wakulima na hata pale ambapo tumenunua tumegubikwa na matatizo ya kuyasafirisha kutoka mahali ambapo pana ziada kutoka huko Nyanda za Juu Kusini kwenda katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba tunaendelea kufanya juhudi ya kuuza baadhi ya mazao yale ambayo tunayo ili tuweze kupata fedha za kununua mazao mingine. Hata hivyo, ninavyozungumza Serikali imeruhusu tani 90,000 ziuze kutoka kwenye maghala yetu, tani 50,000 ziuze kwa Shirika la *World Food Programme* na tani zingine 40,000 tumewaruhusu wafanyabiashara wanunue na wauze nje ili tupate fedha za kuendelea kuyanunua mahindi hayo ambayo bado hayajanunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo Serikali pia inaendelea kutafuta fedha za kununua mahindi hayo na ninavyozungumza pia Serikali sasa hivi inajiandaa, ina-*mobilize* shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kununua mahindi hayo ambayo bado yako mikononi mwa wakulima. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba mahindi hayo yote yanunuliwe na yasafirishwe kutoka huko yaliko yaende kule ambako kuna shida kama Mikoa ya Dodoma na Shinyanga na mahali pengine.

Na. 59

Kuendeleza Uvuvi Mkoani Tanga

MHE. AMINA M. MWIDAU aliuliza:-

Mkoa wa Tanga upo kandokando ya Bahari ya Hindi na hivyo shughuli za uvuvi ni kati ya shughuli kuu kwa wananchi wa Tanga hasa vijana:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuendeleza Sekta ya Uvuvi, Mkoani Tanga?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohamedi Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa Mpango Mkakati wa kuendeleza sekta ya uvuvi nchini ili kuboresha uzalishaji, maisha ya wavuvi wakiwemo vijana na kuongeza pato la Taifa. Mikakati na mipango hii imeainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016 na katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi (*FSDP*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango na mikakati hii inalenga kuendeleza sekta ya uvuvi kwa namna iliyo endelevu. Shughuli zilizopangwa ni pamoja na kuimarisha:-

- (a) Utafiti, Mafunzo na Ugani;
- (b) Miundombinu ya Viwanda, Masoko na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi;

- (c) Ukuzaji Viumbe kwenye maji (*aquaculture*); na
- (d) Uwezo wa kisheria na kitaasisi kwenye sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sehemu ya utekelezaji wa mikakati hii, kati ya mwaka 2008 na 2010, Serikali kupitia Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani (*MACEMP*) imefadhili jumla ya miradi ya kiuchumi 93 kwenye jamii ya wavuvi Mkoani Tanga. Thamani ya miradi hii ni jumla ya shilingi 1,371,935,246/= na mradi huo umewanufaisha takribani wananchi 1,627 wakiwemo vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujengea uwezo sekta ya uvuvi, Mkoani Tanga, mradi huu umenunua na kugawa magari mawili kwa kila Wilaya za Pangani na Mkinga, pikipiki nane kwa kila Wilaya za Muheza mbili, Mkinga mbili, Tanga Mjini mbili na Pangani mbili. Aidha, mradi umenunua boti nne za doria; Pangani moja, Mkinga moja, Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ya Silikati – Tanga moja na Kituo cha Doria Tanga moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mradi umewezesha uanzishwaji wa vikundi 37 vya usimamizi shirikishi wa rasimali za uvuvi yaani *BMUs* na kuvipatia mafunzo. Mradi pia umejenga matanuru mawili ya mifano na kuwafundisha pia wavuvi wa samaki katika maeneo hayo jinsi ya kujenga na kutumia matanuru hayo yaliyoboreshwa.

NAIBU SPIKA: Naona watu wa baharini wote wamesimama, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau!

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa uvuvi ni kati ya shughuli kuu za kiuchumi kwa ukanda wa Pwani na hasa kwa vijana wengi wa ukanda wa Pwani na wavuvi walio wengi ni maskini sana. Ni kwa nini Serikali inapofanya doria na kuwakuta na makosa wavuvi hao huwapiga sana na wakati mwingine mpaka kuuawa kama ilivyotokea Mkoani Tanga Tongoni mwaka 2010? Vilevile huwavunjia vyombo vyao badala ya kuwanyang'anya nyavu ambazo inasemekana kwamba ni haramu na kuwapa nyavu mbadala? Serikali haioni kuwa inawazidishia umaskini wavuvi hao?

Pili, kwa kuwa, katika nchi yetu wafugaji wanajengewa malambo, wanapewa madawa kwa ajili ya mifugo yao, wakulima wanapelekewa Mabwana Shamba, wanapatiwa pembejeo na mbolea na tunafahamu kwamba nchi yetu tuna utajiri mkubwa sana wa bahari kwa mfano *aqua culture*, japokuwa Serikali imeonesha katika mpango mkakati wa uvuvi wa miaka mitano, je, Serikali haioni kuwa ni lini itapeleka wataalam wa uvuvi kwa ajili ya *aqua culture*? Naomba Serikali itamke ni lini mipango ya miaka mitano ni mingi sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lekule Laizer angekuwa na nafasi hapa kwamba wafugaji wanapendelewa kuliko wavuvi sina hakika angejibu vipi.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu kwa maswali ya Mheshimiwa Amina Mwidau.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, moja, tuelewe vizuri kwamba lengo la kuharamisha uvuvi wa baadhi ya samaki lakini pia utumiaji wa baadhi ya nyavu na vifaa vingine lengo ni ili kuhakikisha kwamba uvuvi unabaki kama kitu endelevu. Lakini pili, niseme kwamba sina uhakika kama watu wanaosimamia taratibu hizi za kuhakikisha kwamba uvuvi haramu haufanyiki kwenye maeneo husika, kama wamejichukulia sheria mikononi mwao. Kama wamefanya hivyo ni kosa na ningemwomba Mheshimiwa Mbunge Mwidau atupe taarifa za uhakika ili tuweze kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba pamoja na uhitaji na umaskini hatuwezi tukaruhusu sheria kuvunjika ili kuhalalisha jinsi watu watakavyojipatia kipato na Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake za mwaka 2009 hasa kanuni ya 59 mpaka 66, zimekuwa wazi kabisa kwamba, ni aina gani ya nyavu zinazoruhusiwa, vitu kama matumizi ya sumu hayaruhusiwi, matumizi ya makombora pia hayaruhusiwi na ni vizuri Mheshimiwa Mbunge tukatafuta namna ya kuwawezesha watu hawa wale

wavuvi wadogowadogo lakini kwa namna ambayo haitavunja sheria na haitaleti athari katika jamii inayotumia samaki na mazao ya samaki.

Ni kweli kama anavyosema kwenye swali lake la pili kwamba, wakulima na wafugaji wanajengewa miundombinu, lakini ni vizuri tu pia Mheshimiwa Mbunge naye akafahamu kwamba ukienda Ziwa Viktoria na hata katika Mikoa hii minne yenye huu mradi wa MACEMP kama Tanga, Pwani, Dar es Salaam na Lindi kumekuwepo pia na ujenzi wa miundombinu ili kuwawezesha na kuwasaidia wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hawa watu wanaojihusisha na *aquaculture* wamewahi kupelekwa nje na kuna watu walitoka Kagera wakapelekwa Vietnam kwa ajili ya kujifunza mbinu mpya za kuweza kufanya ufugaji huo wa samaki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, sasa naona wengine wanasimama sijui kama ni wavuvi, lakini basi tusikie swali kutoka kwa wavuvi wa Mpanda Mjini na swali la mwisho litakuwa kutoka kwa Mheshimiwa Dustan L. Kitandula. Mheshimiwa Said Amour Arfi!

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, uvuvi hauko katika bahari kuu peke yake. Je, Serikali imefanya mikakati gani kuwasaidia wavuvi wadogowadogo katika Maziwa ya Viktoria na Tanganyika? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyogusia kwa upande wa Ziwa Viktoria, kumekuwepo na mradi uliowasaidia sana wavuvi kujenga mialo lakini kuwaweka pia katika makundi yaliyopata fedha kuwezesha kuweza kuvua kwa namna nzuri zaidi. Kwa kweli wengi wameweza kujipanga vizuri kwenye Mikoa ya Mara-Musoma, Mwanza na Kagera na ndiyo maana hata sasa katika Ziwa Viktoria wameweza kuvuna hata kupita kiasi na kiasi cha samaki wanaopatikana hasa sangara kwa sasa viwanda vilivyopo Kagera na Tanga vyenye uwezo wa ku-process tani 60,000, hivi vimekuwa vina-process tani 10 tu kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ziwa Tanganyika kuna mradi pia wa kimazingira wenye mabilioni ya dola unaozihusisha nchi za Tanzania, Burundi, Kongo na Zambia na huu kwa kweli pia umejipanga ili kuweza pia kuwawezesha na kuwajengea uwezo wavuvi wadogo wadogo hasa waliopo kando ya Ziwa Tanganyika.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali kupitia MACEMP imetumia fedha nyingi sana, lakini kwa bahati mbaya mradi ule haukuweza kuwaondoa wananchi kwenye umaskini. Je, ni lini sasa Serikali itakuja na mradi utakaowawezesha wavuvi wa ukanda wa Pwani kuondokana na uvuvi wa kizamani ili waweze kutumia boti za kisasa lakini vilevile waweze kufuga samaki kwenye maeneo yao ya mwambao wa Pwani?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, moja, mpango tunaotumia kwenye maendeleo ni *D by D* yaani *Development by Devolution* na hivyo Mheshimiwa Mbunge kuuliza kwamba Serikali ni lini itakuja na mpango, nibadilishe tu kwamba Serikali ipo tayari lakini tusaidiane na Mheshimiwa Mbunge kuibua miradi kutoka kwenye vijiji na waliko watu ili kuhakikisha kwamba miradi hiyo itajibu mahitaji yao halisi na huo usije pia ukaonekana kwamba ni hasara kama huo anaouona kama ni hasara, lakini sisi tunauona kwamba ni mradi ambao umekuwa na mafanikio mengi. Ppia tusaidiane katika kuhamasisha kuwaweka watu katika makundi ya uzalishaji yanayoweza kupata mikopo ili vifaa hivyo alivyogusia vya kuvulia waweze kuvipata hao watu wanaovua katika ngazi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na sasa tuhamie katika Wizara ya Maliasili na Utalii, swali la kutoka kwa Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo.

Na. 60

Kuboresha Pori la Akiba Pande

MHE. JOHN J. MNYIKA aliuliza:-

Pori la Akiba la Pande liko kwenye Jimbo la Ubungo katika Manispaa ya Kinondoni:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiweke miundombinu na vivutio mbalimbali ili pori hilo liweze kuhudumia watu na kuanzisha utalii ambao utaongeza mapato ya Taifa na ajira kwa wananchi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha hadhi pori hili ili liweze kutumika pia kwa shughuli za utafiti?

(c) Je, wananchi wanaoishi jirani na pori hilo wanafaidikaje na uoto wa asili, maliasili na rasilimali za pori hilo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imeanza mkakati wa kuboresha miundombinu ya pori la Pande kwa kulima kilomita zote 15 za mpaka na kilomita 30 za barabara za ndani ambazo kwa sasa zinapitika kwa mwaka mzima. Pia imeanza kutengeneza *culvert* mbili katika mpaka wa Kijiji cha Msakuzi na kujenga nyingine moja katika mpaka wa Kijiji cha Mpigi Magohe. Pia ujenzi wa ofisi na nyumba moja ya matumizi unaendelea. Aidha, Wizara inaendelea kutenga bajeti ya ukarabati wa barabara na mpaka wa pori hilo kila mwaka. Mipango ya baadaye ya Wizara ni pamoja na kutengeneza uzio, kuchimba mabwawa ya maji na kupandikiza wanyama watakaokuwa kivutio kwa wananchi na wageni wengine watakaotembelea pori hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara haina mpango wa kulipandisha pori hilo kwa sasa licha ya kutokuwepo kwa mpango huo kwa wakati huu, Taasisi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali zimekuwa zikiendelea kufanya tafiti mbalimbali za wanyama, mimea, ndege na baionuai katika pori hilo kwa muda mrefu. Kwa mfano, Shirika Lisilokuwa la Kiserikali la *Tanzania Forest Conservation Group* kwa kushirikiana na Wizara, *Wildlife Conservation Society of Tanzania*, *Misitu Yetu Project* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamewahi kufanya tafiti kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinalitumia eneo hilo kwa tafiti zao na vilevile wanalitumia kama eneo la kujifunzia kwa wanafunzi wao yaani *Study Area* na kwa mfano, mwaka huu peke yake Wahadhiri wawili kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamefanya mazoezi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwanufaisha wananchi na kufanya waweze kufaidika na maliasili zilizopo katika maeneo yao limeainishwa vizuri katika sera ya wanyamapori ya mwaka 1998 iliyoarekeshwa mwaka 2007 ambayo inatoa kipaumbele katika kushirikisha wananchi katika uhifadhi.

Hata hivyo, kwa sasa Wizara yangu bado inaboresha miundombinu ya pori hilo ili kulirejesha katika hali stahiki ya kihifadhi kabla ya kuanzisha mipango ya kimatumizi ya biashara itakayotengeneza fedha nyingi zitakazoweza kusaidia miradi mingi ya wananchi. Katika hatua hizi za awali, baadhi ya wananchi wa vijiji vinne vinavyozunguka pori wanafaidika kwa ajira za mara kwa mara za ukarabati wa mpaka ambapo mwaka 2010 wananchi 20 walijajiriwa kwa muda na mwaka huu pia wananchi 12 wameajiriwa kwa muda kushiriki katika shughuli za uhifadhi na usimamizi wa maliasili zilizopo kwenye bonde hilo kutoka vijiji ya Mbopo, Msumi, Msakuzi na Mpigi Magohe.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwanza naomba azingatie kwamba maeneo yote hayo siyo vijiji ni mitaa na yako ndani ya Manispaa ya Kinondoni.

Sasa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: Maelezo ambayo yametolewa yanaonesha kwamba, pori hili ambalo lina *square* za mraba zaidi ya 1,000 halitumiki vizuri na pori hili

lilianzishwa toka mwaka 1952, wakati linaanzishwa lilikuwa na wanyama wakiwemo Simba na Faru. Sasa hivi limebaki na wanyama wadogowadogo tu na mimea species takriban 400. Je, Serikali iko tayari, maana kadri tunavyozidi kuchelewa wanyama wanazidi kupotea na species zinazidi kupotea? Je, Serikali ipo tayari kuweza kuharakisha mpango wa kulifanya hili eneo kuwa *park* kwa maana ya *park all zone* kama ambavyo Miji mingine kama Nairobi na Miji mingine duniani ilivyotengeneza *park* kwenye Majiji yake na kutengeneza mapato makubwa ya Serikali pamoja na ajira?

Swali la pili, kwa kuwa, kwenye sehemu (c) ya majibu yake, Mheshimiwa Waziri amezungumza kuhusiana na haja ya kushirikishwa kwa wananchi. Kwa kuwa, pamekuwepo na migogoro mikubwa ya kimipaka baina ya wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi na Mamlaka za hifadhi kama ilivyotokea Meatu na Urambo ambapo wananchi walivunjiwa nyumba na nyumba zao kuchomwa moto na mali zao kuharibiwa. Je, Mheshimiwa Waziri anawahakikishiaje wananchi wa Manispaa ya Kinondoni na Jimbo la Ubungo katika maeneo ya Mbopo, Msumi, Mpiji Magohe pamoja na Msakuzi kwamba hapatakuwa na migogoro ya mipaka katika maeneo yao kama ambavyo Serikali imeshindwa kushughulikia migogoro ya mipaka kwenye maeneo ya Meatu, Urambo na maeneo mengine ya nchi yetu?

NAIBU SPIKA: Majibu Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ni kweli kabisa Pande inaweza kuwa ni sawasawa na *Nairobi National Park*.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa John John Mnyika kwa kutoa mawazo mazuri sana ya kusaidia katika uboreshaji wa pori hili na kullitumia kwa ajili ya kibiashara. Lakini pia niombe tu kusahihisha kidogo kwamba pori hili la Pande lina kilomita za mraba 15.7 na si 1,600.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya masahihisho hayo naomba tu kusema kwamba, mpango wa Serikali kupitia Sheria ya Wanyamapori namba tano ya mwaka 2009 ni kushirikisha sekta binafsi katika mpango unaoitwa PPP ili kuweza kullitumia eneo hili kibiashara. Changamoto ambayo tumekuwa nayo kama Serikali kwa kweli ni fedha, ili kuweza kullilinda vizuri kwa maana ya kuliwekea uzio na ku-introduce wanyama zinahitajika fedha nyingi sana ambazo kwa bajeti ya kawaida ya Serikali siyo rahisi kuzipata. Kwa hiyo, tunashirikisha sekta binafsi katika uhifadhi na tumekwishaanza taratibu za kuelekea kwenye hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kuhusu suala la mpaka kama alivyosema, kwa sasa hatuna migogoro ya mipaka kwenye maeneo, bahati nzuri kwa sababu ni eneo dogo na mipaka yake inajulikana. Hata hivyo tumekuwa tukishirikiana na wananchi wa maeneo hayo mara kwa mara kwa maana ya kuzungumza na kuonesha maeneo ambayo mipaka inatakiwa kuwa. Pia kwa sababu bado mipaka yenyewe haijawa wazi sana kwa sababu ya kutokuweka uzio ndiyo maana tumeanza kuilima mwaka huu ili iweze kuonekana vizuri zaidi.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Jiji la Dar es Salaam ni kioo cha nchi yetu, sehemu ambayo ingeweza kuwa kivutio kikubwa kwa ajili ya utalii, lakini Serikali imekuwa ikibomoa majengo ya kihistoria kama vile Saramanda. Sasa napenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri je, Serikali ina vivutio gani katika Mji wetu wa Dar es Salaam au ina mikakati gani ya kujenga vivutio vya utalii ukiachilia mbali *fish market* ambayo kwa sasa hivi ni chafu na imekufa?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa uendelezaji wa utalii wa Kikanda, Jiji la Dar es Salaam limekwishaunda Bodi yake ya Utalii yaani Dar es Salaam *Tourism Board* ambayo inashirikiana na Bodi ya Utalii ya Wizara, katika kuendeleza utalii na kuna baadhi ya maeneo ambayo yameshaainishwa tayari. Baadhi ya maeneo kama alivyosema *Fish Market* lakini vilevile kuna soko kuu la Kariakoo, kuna Shule ya Sekondari ya Pugu, nyumba ya Mwalimu iliyopo Magomeni pamoja na maeneo mengine ikiwemo pia sehemu ambayo wanauza vinyago Mwenge. Kwa ujumla yapo maeneo kadhaa ambayo yameshaainishwa na taratibu za kuyatangaza na kuyaweka kwenye mpango wa utalii wa Jiji zinaendelea.

MHE. SULEIMAN S. JAFU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa unapozungumzia mapori kwa Tanzania huachi kuzungumzia msitu wa Kazimzumbwi na Ruvu Chini na kwa kuwa, misitu hii kila

mwaka inaendelea kuharibika: Je, Serikali ina mipango gani sasa kuhakikisha vijana waliohitimu mafunzo ya mgambo kutoka Kijiji cha Kisarawe na Kijiji cha Masaki waweze kuchukuliwa kwa ajili ya suala zima la ulinzi shirikishi katika maeneo haya na kupata ajira?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jafo, naomba nimshukuru sana kwa kuona umuhimu wa kuhifadhi misitu hii ya Ruvu Chini, Ruvu Kaskazini pamoja na Kazimzumbwi. Wizara, ili kuimarisha ulinzi wa misitu imekwishaanzisha Wakala wa Misitu toka mwaka jana, 2011 Wakala ambao utakuwa na uwezo mzuri zaidi wa kifedha zaidi ya Idara ilivyokuwa, na tayari zimekwishakutengwa fedha kwa ajili ya kuanza kuajiri baadhi ya askari walinzi wa misitu, yaani *Forest rangers* ambao watakuwa wanaajiriwa kutoka kwenye maeneo ya vijiji ambao misitu hiyo ipo. Kwa sababu mpango huu ndiyo tumeanza, nimhakikishie tu kwamba tutawashirikisha wananchi wa maeneo hayo na kwa uhakika vijana wake ambao anawazungumzia, tutakuwa tunawapa ajira za muda kutegemea na upatikanaji wa fedha.

Na. 61

Mpango wa Kuongeza Majengo Kitengo cha MOI – Muhimbili

MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.N.Y. MHE. RITA L. MLAKI) aliuliza:-

Kuna wagonjwa wengi sana wanaougua magonjwa ya mgongo, (*disc*) na mishipa ya fahamu (*nerves*) ambayo imesababisha watu wengi kushindwa kutembea na maumivu makali; na Serikali inakusudia kuongeza majengo kwenye Kitengo cha MOI – Muhimbili:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kuanza ujenzi huo, na ni lini ujenzi huo unategemea kukamilika?
- (b) Kwa kuwa, Wataalam wa Mishipa *Neuro-Surgeon* ni wachache sana kwa nchi nzima: Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongeza wataalam hao?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki - Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2011/2012 imetoa Shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya litakalotumika kwa ajili ya upasuaji wa mishipa ya fahamu (*neuro-surgery*). Ujenzi wa jengo hili utagharimu Shilingi bilioni 17.9. Fedha hizi tayari zimepatikana kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya baada ya Serikali kuridhia na kutoa dhamana. Ujenzi utaanza mwezi Mei, 2012 na utachukua muda wa miezi 24 (miaka miwili) na Mkandarasi tayari amekwishaapatikana.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa wataalam, Serikali imefanya juhudi za kuongeza wataalam wa mishipa ya fahamu (*Neuro-surgeons*) kwa kugharamia mafunzo ya wataalam wane. Wataalam hawa wanapata mafunzo kwa ushirikiano kati ya MUHAS, Afrika Kusini na Misri. Mafunzo ya wataalam wanaohitajika yanafanyika hapa nchini, ili kupunguza gharama za mafunzo na kuongeza idadi ya wataalam wanaoweza kusomesha. Suala la kusomesha wataalam adimu kama hawa ni ajenda ya kudumu katika Wizara yangu mpaka hapo watakapopatikana wataalam wa kutosha.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa maradhi haya ya uti wa mgongo hivi sasa ni tishio kwa Watanzania wengi na hasa kutokana na haya masuala ya ajali nyingi, mambo ya *stroke* na kadhalika: Je, Serikali iko tayari kuboresha huduma za vitengo vya *physiotherapy* vilivyoko katika Hospitali za Mikoa na Rufaa hasa Mkoani Mbeya, Dodoma na kadhalika hasa katika maeneo ya vifaa pamoja na wataalam?

Swali la pili, kwa kuwa Waziri anatuambia hapa wataalam ni wachache: Je, Serikali iko tayari kuanzisha Kitengo cha Mafunzo kwa wana-*physiotherapy* katika Chuo Kikuu cha Tiba cha Muhimbili badala ya kutegemea KCMC peke yake? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vitengo vya *physiotherapy*, yaani mazoezi ya viungo bado havijaimarika kwenye hospitali zetu za Mkoa. Lakini kwa sababu Serikali sasa imeamua kwamba hospitali hizi zitakuwa ni Hospitali za Rufaa tumeona kwamba iko haja ya kuongeza udahili kwa ajili ya mafunzo ya *physiotherapy* ili tuweze kupata wataalam wengi wa kupeleka kwenye hivi vitengo kwa sababu hii ni huduma ambayo ni muhimu pia ambayo inahitaji bingwa anayeweza kufanya kwa utaalim zaidi. Tunaendelea kuhakikisha kwamba hawa wanapatikana kwa wingi na vitengo vinaimarishwa katika Hospitali za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kweli kwamba mpaka sasa hivi mafunzo ya mazoezi ya viungo yanatolewa katika Hospitali ya KCMC tu. Lakini tumeona kwamba iko haja ya kuhakikisha kwamba vyo vyetu vingine hapa nchini hata vyo vya *Private* tunavi-*encourage* kwamba waanzishe kwa sababu bado soko la wataalam hawa ni kubwa na wanahitajika. Naomba kusema kwamba namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutukumbusha kwamba iko haja ya kuongeza chuo. Naomba atuvumilie, tutaangalia namna ambavyo tunaweza tukaongeza Chuo kingine ili tuweze kupata wataalam wa kutosha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Kwa sababu ya muda, Waheshimiwa nawaombeni mniwie radhi kidogo. Sasa Wizara ya Nishati na Madini, swali la Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mbunge wa Serengeti.

Na. 62

Hitaji la Umeme Serengeti

MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.N.Y. MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE) aliluliza:-

Umeme wa Gridi ya Taifa umefika Wilaya ya Tarime (Nyamongo) ambayo ipo jirani na Wilaya ya Serengeti, zimetenganishwa na Mto Mara:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha umeme huo Wilayani Serengeti kwa kufanya "Looping" kutokea Nyamongo?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo itarahisisha umeme kupelekwa katika Tarafa ya Rogoro, Ikorongo na Ngoreme?
- (c) Je, Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo itasaidia maeneo ya Rung'abure, Nyamoko, Matare na Burunga kupata umeme wa *three phase* badala ya *single phase* kama ilivyo sasa?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kufikisha umeme Serengeti kutokea Nyamongo ni Shilingi bilioni 3.3. Gharama hizo zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa KV 33 pamoja na usambazaji wa umeme katika Vijiji vya Kewanja, Kerende, Murito 1, Murito 2, Mara Centre, Nyasurura, Kitarungu, Rung'abure, Nyamoko na Matare. Serikali kupitia TANESCO imewasilisha maombi ya fedha za utekelezaji wa mradi huu kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na punde fedha zitakapopatikana ujenzi utanza mara moja.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa kuunganisha Wilaya ya Serengeti kutoka kwenye Kituo cha Nyamongo, mbali ya kuboresha upatikanaji wa umeme Wilayani Serengeti pia kutarahisisha

usambazaji wa umeme katika maeneo mengine aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Fedha zitakapopatikana, Serikali itaanza utekelezaji wa mradi huo kama tulivyoeleza.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa kujenga njia hii mbadala ya kufikisha umeme Serengeti, kutaboresha upatikanaji wa umeme katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Kama nilivyoeleza awali, TANESCO imewasilisha maombi ya utekelezaji wa mradi huu REA, hivyo tunaomba subira wakati Serikali ikitafuta fedha za kutekeleza mradi huo.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ambapo nina imani kabisa Dkt. Kebwe atayafurahia. Hata hivyo, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali kupeleka umeme katika maeneo mapya hapa nchini kwa mikakati mbalimbali, bado kuna matatizo makubwa ya mgao wa umeme. Serikali inasema nini kuhusu tatizo hili la mgao wa umeme kupunguzwa badala ya kuendelea na maeneo mengi zaidi wakati uwezo wa kufikisha umeme ni mdogo kitaifa?

Pili, ni matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza nchi nzima ya kukatika kwa umeme kutokana na msongamano mkubwa na matumizi makubwa ya umeme, kwa mfano, katika Wilaya ya Muheza kwa muda wa miezi mitatu sasa hatujapata umeme, kila siku *transfoma* zinaungua: Je, kuna mkakati gani wa kuondoa matatizo haya makubwa kitaifa?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mikakati iliyopo ya kudhibiti na kuimarisha huduma ya umeme inakwenda sambamba kwa maana ya maeneo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji.

Katika hali ambayo tuliyokuwa nayo kwa muda mrefu ya kuwepo kwa mgao wa umeme sote tumeshiriki kwa pamoja likiwemo Bunge hili Tukufu kuweka mikakati ya pamoja, pamoja na wataalam wa nchi hii na hali tuliyonayo leo kwa maana ya uzalishaji imefikia mahali pazuri. Uwezo wa kuzalisha umeme kwa hali tuliyonayo kwa tathmini ya mahitaji ambayo wanasema ni *suppressed demand*, tuna uwezo wa kuzalisha umeme kuliko mahitaji ya siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu kukatika kwa umeme, hali iliyopo sasa hivi ni kwamba iko miradi mingi kwanza ya kuboresha miundombinu yetu tuliyokuwanayo, lakini pia na kuongeza maeneo ya usambazaji umeme na kuboresha huduma ambazo zimekuwa zikitolewa na TANESCO kwa maana ya kuwafikishia wateja huduma iliyo bora kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Watanzania kwa ujumla kwamba juhudi zinazofanyika pamoja na kuboresha miundombinu ya kusafirisha, lakini pia tunaboresha miundombinu ambayo inawezesha kuwafikishia wananchi umeme na pia wakati huo huo tutaendelea kusambaza umeme kwa sababu tunaamini kwamba umeme utachangia kuboresha na kuimarisha uchumi wa Taifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mkitazama saa zetu kushoto kabisa, na bado nina maswali kadhaa, mniwie radhi. Sasa tumpe nafasi Mheshimiwa January Yusuf Makamba - Mbunge wa Bumbuli kwa Wizara hiyo hiyo ya Nishati na Madini.

Na. 63

Ukosefu wa Umeme Kata ya Vuga

MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA (K.N.Y. MHE. JANUARY Y. MAKAMBA) aliuliza:-

Kata ya Vuga katika Jimbo la Bumbuli haina umeme licha ya kuzungukwa na maeneo yenye umeme:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye Kata ya Vuga?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa tulizonazo Jimbo la Bumbuli lina Kata 16. Kati ya hizo, Kata tisa tayari zina umeme wa uhakika. Kata saba kati ya hizo ikiwemo Kata ya Vuga ndizo ambazo bado hazijafikishiwa huduma hiyo ya umeme. Umeme katika Kata ya Vuga utatokea kwenye Kata ya jirani ya Soni iliyoko umbali wa kilometa 8.154. Mradi huo utagharimu Shilingi milioni 568 na utahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 11 yenye urefu wa km. 8.5, laini ya usambazaji umeme wa msongo wa KVA 400 yenye urefu wa km 10 pamoja na kufunga *transfoma* mbili zenye uwezo wa KVA 25 kila moja, tatu (3) zenye uwezo wa KVA 50 kila mmoja na moja, yenye uwezo wa KVA 10. Mradi huu unafadhiliwa na TANESCO na utekelezaji wake umeshaanza kwa kufanya *survey* ambayo ilikamilika tarehe 27 Januari, 2012 na mafundi wanajiandaa kwenda *site* kuanza kazi ya ujenzi kwa kuanza na usimikaji wa nguzo ambao unatarajiwa kuanza mwezi huu wa Februari, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Makamba kwa ufuatiliaji wake kama wanavyofanya Waheshimiwa Wabunge wengine.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii kuwapongeza watani zetu Chama cha Mapinduzi kwa kusherehekea miaka 35 jana. (*Makofi*)

Pili, nina swali dogo tu la nyongeza. Serikali imefikia wapi katika mradi wa kusambaza umeme katika Jimbo la Kigoma Kaskazini ambao unaonekana katika bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini mwaka huu?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zitto anafuatilia miradi katika Jimbo lake, tulijibu na tulitoa maelezo mwaka jana na anafahamu kwamba makadirio yaliyofanywa mwaka ule ni Shilingi bilioni 5.5 na sasa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine mradi mkubwa wa kuwafikishia Watanzania huduma ya umeme unaofanana ambao sasa hivi unatekelezwa katika Mikoa 16, taratibu za kuwapata makandarasi zinaandaliwa na tunatarajia inapofika mwezi Machi au Aprili mwaka huu, tenda zitakuwa zimeshatangazwa ili tuingie tena kwenye awamu nyingine ya mradi mkubwa wa kuwafikishia Watanzania wengi huduma ya umeme pamoja na Jimbo la Mheshimiwa Zitto.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, bado nina maswali manne. Tunahamia Wizara ya Maji.

Na. 64

Mfumo wa Ulipaji Maji Nchini

MHE. MARIAM R. KASEMBE aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka kwa Mamlaka za Maji nchini kutumia mfumo wa *Pre-paid* kulipia bili za maji ili kudhibiti upotevu holela wa maji kama ilivyo kwa Uganda na Mkoa wa Dodoma ambapo wameanza kutumia utaratibu huo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaotumika sasa wa kulipia ankara za huduma ya maji ni kwamba mteja analipia huduma baada ya matumizi. Mfumo wa *Pre-paid* ni utaratibu ambao analipia huduma kabla ya matumizi (ananunua huduma). Mfumo huu unasaidia sana kwa mteja kudhibiti

matumizi yake ya maji na pia kugundua uvujaji unaotokea. Kwa upande mwingine mfumo wa *Pre-paid* unasaidia Mamlaka kukusanya maduhuli yote ya maji yaliyouzwa, kupunguza wizi wa maji na mfumo huu pia unaweza kupunguza idadi ya wasomaji wa mita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa *Pre-paid* wa kulipia ankara za maji ni teknolojia mpya ambayo kwa sasa imeanza kutumika katika nchi kadhaa duniani. Katika kuboresha utoaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma iliamua kujaribu mfumo huo na kutathmini matokeo yake. Mwezi Agosti, 2009 Mamlaka hiyo ya Majisafi na Majitaka iliagiza dira za maji 100 za mfumo wa *Pre-paid* kutoka Afrika ya Kusini kwa majaribio ili kuangalia ubora wake katika kudhibiti upotevu holela wa maji uliokuwepo. Mpaka sasa Mamlaka imefunga dira kwa wateja 400 na lengo ni kuwafungia wateja wote 23,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya matokeo mazuri ya Mji wa Dodoma, Serikali itaendelea kuhamasisha Mamlaka zote nchini ziweze kutumia teknolojia ya mfumo wa *Pre-paid* kulipia ankara za maji ili kudhibiti upotevu holela wa maji na wizi wa maji.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa watumiaji wengi wa maji Mijini wamekuwa wakilalamika sana juu ya bili kubwa wanazopelekewa hata kama maji hayo hayatoki au tofauti na kiwango cha maji wanachokitumia; na kwa kuwa Mji wa Masasi unatarajia kuwa na maji ya kutosha, chanzo cha maji Mbwinji pindi kitakapokamilika: Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuanzisha mpango huu katika Mji wa Masasi ili Maji Mbwinji yatakapopatikana uendane sambamba na mpango huo wa wananchi ili waweze kutumia kufuatana na matumizi ya maji wanayoyatumia?

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekuwa na ahadi ya kuja Jimboni kwangu Wilaya ya Masasi kwa muda mrefu sana na hajafanya hivyo: Je, haoni ipo haja sasa ya kutimiza ahadi hiyo kwa haraka ili kuja kuangalia tatizo kubwa la maji lililopo katika Vijiji vya Jimbo langu la Masasi na ili uweze kupata fursa ya kuongea na Bodi ya Maji Masasi kuwaelezea mpango huu mzuri na sisi tuweze kuutekeleza katika Wilaya yetu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Mariam Kasembe kwa kuleta wazo hili la kuhamasisha Mamlaka zetu kutumia mfumo wa *Pre-paid*. Huu mfumo utatuondolea ugomvi wanaolalamika sasa kwamba bili zinakuwa kubwa, labda maji hayatoki, lakini kama umelipa *Pre-paid*, hilo tatizo litakuwa hakuna. Kwa hiyo, nina uhakika kabisa kwamba Miji yote tunaihamasisha pamoja na Mamlaka ya Masasi baada ya kuboresha Mradi huu wa Mbwinji waanze kutumia mfumo wa *Pre-paid*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu swali lake la pili, naomba nimwahidi kwamba kipindi hiki kabla ya Bunge lijalo nitakuwa nimefika Masasi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa kweli muda ni mdogo sana naomba mniwie radhi sana. Twende swali Na. 65 la Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo - Mbunge wa Liwale.

Na. 65

Matatizo ya Maji Kijiji cha Kichonda

MHE. FAITH M. MITAMBO aliuliza:-

Kijiji cha Kichonda Wilayani Liwale kimekuwa na matatizo ya maji kwa muda mrefu, licha ya kuwa kwenye mradi wa *World Bank* na ahadi ya kukipatia kijiji hicho maji:-

(a) Je, ni lini mradi wa *World Bank* utachimba kisima kwa ajili ya wanakijiji hao?

(b) Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwapatia maji wananchi wa Kichonda itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faith Mitambo, Mbunge wa Jimbo la Liwale lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kuboresha huduma ya maji katika Kijiji cha Kichonda. Mwaka 2004/2005 Serikali kwa kushirikiana na JICA ilichimba kisima kirefu katika Kijiji hicho, lakini hakikuwa na maji. Mwaka 2006/2007 kilichimbwa kisima kingine kirefu kupitia Mradi wa TASAF ambacho pia hakikuwa na maji. Utafiti wa maji ardhini kupitia mradi wa vijiji 10 nao haukuwa na mafanikio. Juhudi zilifanyika pia kuangalia uwezekano wa kupata maji kutoka vijiji jirani vya Mbuli na Nyera vinavyotekeleza Mradi wa Vijiji 10, lakini visima hivyo vilivyochimbwa havikuweza kuwa na maji ya kutosha na kuwapatia wananchi wa Kichonda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Kijiji cha Kichonda hakikufanikiwa kupata maji ya ardhini katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mradi wa vijiji 10, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale imeweka mipango ya muda mfupi kutatua tatizo la maji Kijijini humo. Mipango hiyo ni ya kuvuna maji ya mvua kwenye Zahanati ya Kichonda ambapo Shilingi milioni 20 zimetengwa kupitia Mfuko wa TASAF. Mpango wa muda mrefu uliopo ni kufanya usanifu wa kina na kutumia njia mbadala kama ujenzi wa mabwawa kuwapatia wananchi wa Kijiji cha Kichonda huduma ya maji ya uhakika. Mpango huo utafanyika katika awamu ya pili ya programu itakayoanza mwaka 2013/2014.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa mpango wa kuvuna maji ya mvua katika Zahanati ya Kichonda ni Mpango wa muda mfupi na kwa kuwa Kijiji cha Kichonda ni kijiji kikubwa na kina wakazi wengi na nina uhakika kabisa kwamba kwa mpango huu uliobuniwa sasa hauwezi kutoshereza kijiji kile: Je, Serikali haioni umuhimu wa kuchukua hatua za ziada zaidi ili kijiji hiki kiweze kupatiwa maji?

Swali la pili, kwa kuwa imeonekana ufumbuzi wa sasa unaotakiwa kuchukuliwa ni kuchimbiwa mabwawa katika kijiji hiki na kwa kuwa wakazi wa Kijiji cha Kichonda wameshaahidiwa na wameshaanza kupatiwa maji kwa muda mrefu bila mafanikio: Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia sasa mabwawa haya yanayotarajiwa kuchimbwa yatachimbwa katika maeneo gani na ni Shirika gani litafanya kazi ya kuchimba mabwawa haya na utekelezaji wa mradi huu utategemea kuanza lini na unategemea kukamilika lini? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, kijiji kile tumeshindwa kupata maji chini ya ardhi na tukafikiria kwamba *option* ambayo tunaweza kufanya kwa mpango wa muda mfupi ni kuweza kujenga mfumo wa kuvuna maji ya mvua. Nikasema ya kwamba, katika mpango wa muda mrefu ambao tunataka tuingize kwenye programu, tutajenga mabwawa kwa sababu hakuna namna nyingine.

Sasa nimhakikishie Mheshimiwa Faith na Wananchi wa Liwale kwamba, katika programu ya maji awamu ya pili tutawekea mkazo. Kwa hiyo, Serikali kwa kupitia hii WSDP tutajenga mabwawa hayo na hiyo programu itaanza mwaka 2013/2014 kwa sababu awamu hii ya kwanza tumeongeza mwaka mmoja mpaka Juni, 2012. Sasa baada ya hapo sasa tutaainisha maeneo, maana lazima tufanye usanifu na siwezi kutaja vijiji kwamba wapi tutachimba mabwawa. Lazima tufanye usanifu halafu tutashirikiana na Halmashauri ya Wilaya tuweze kupata maeneo ya kuchimba mabwawa kwa wananchi wa maeneo yale.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, bado nina maswali mawili, mniwie radhi kweli. Wizara ya Fedha Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mbunge wa Kojani.

Na. 66

Zanzibar Kuwa Mwananchi wa Benki Kuu

MHE. HAMAD ALI HAMAD (K.N.Y. MHE. RASHID ALI OMAR) aliuliza:-

(a) Kuna taarifa kwamba Serikali ya Zanzibar ni mteja (mwanachama) wa mwanzo wa Benki Kuu ya Tanzania. Je, Tanzania Zanzibar imeshawahi kupata hisa zake kupitia Benki Kuu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mbunge wa Kojani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu ya Tanzania ilianzishwa mwaka 1965 chini ya Sheria ya Bunge, yaani *The Bank of Tanzania Act, 1965* ikiwa ni chombo kinachomilikiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Chini ya Sheria hiyo, hisa zote zilimilikiwa kama ambavyo bado zinaendelea kumilikiwa na Jamhuri ya Muungano ambayo inaundwa na Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Hili limeanishwa pia katika Sheria ya sasa ya Benki Kuu, yaani *The Bank of Tanzania Act, 2006*.

Mtaji ulioanzisha Benki Kuu ilipoanza shughuli zake mwaka 1966 ulitolewa na Hazina ya Jamhuri ya Muungano na mwenye dhamana ya hisa hizo, kama ilivyo kwa mashirika yote ya umma ni Msajili wa Hazina, yaani *The Treasury Registrar*. Kifungu cha 14(2) cha Sheria hiyo iliyoanzisha Benki Kuu kinaelekeza wazi kwamba ni Jamhuri ya Muungano pekee ndiyo inaweza kisheria kumiliki hisa za Benki Kuu. Kifungu hicho kinaeleza kwa lugha ya Kiingereza ambayo kwa ruhusa yako naomba kunukuu:

"The capital of the Bank shall be subscribed and held by the United Republic". Mwisho wa kunukuu. Maana yake ni kuwa ni Jamhuri ya Muungano pekee ndiyo itakayotoa na kumiliki mtaji wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba chini ya Sheria iliyoanzisha Benki Kuu na kama ilivyo kwa Benki Kuu zote duniani, wateja wakuu wa Benki Kuu ni Serikali na mabenki. Hivyo basi, hapa nchini kwetu wateja wakuu wa Benki Kuu ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wateja wengine ni mabenki ya biashara yaliyopewa leseni kuendesha shughuli zake hapa nchini.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kama ni hivyo, mbona nyaraka mbalimbali zinasema kwamba Zanzibar ina hisa asilimia 11.5 iliyotokana na iliyokuwa *East African Currency Board* ambapo Zanzibar ilikuwa ni mwanachama kamili?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kihistoria kulikuwa na hisa ambazo *Republic of Zanzibar* ilikuwa imepeleka kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki ambayo ni hiyo asilimia 11 ambayo ilihamishwa wakati wa kuanzisha Benki kuletwa Hazina ya Jamhuri ya Muungano.

Sasa wakati inaanzishwa, Benki Kuu ilianzishwa kwa ajili ya Serikali ya Muungano. Kwa hiyo, Zanzibar ndani ya muungano inahusika na Benki Kuu. Lakini hisa za asilimia 11 haziko wazi. Hii ni moja katika hoja ambazo Kamati ya pamoja ya Serikali ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea kuizungumza. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Hamad afanye subira ili baada ya mazungumzo, hili litajulikana.

Na. 67

Ubadilishaji wa Umiliki wa Biashara

MHE. CHIKU A. ABWAO aliuliza:-

Kumekuwa na mchezo wa wawekezaji toka nje kubadilisha umiliki wa biashara ile ile kama ilivyofanyika kwa Hoteli ya *Sheraton*, *Royal Palm* kuwa *Movenpick*, Kampuni ya Simu ya *Celtel*, *Zain* na sasa hivi inaitwa *Airtel*:-

Je, katika ubadilishaji huu wa kibiashara, nchi yetu imepata stahiki yake ya kweli kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Chiku Alfan Abwao, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Kampuni kuuzwa kwa Kampuni nyingine au kumiliki hisa za Kampuni nyingine ni la kawaida katika taratibu za biashara za kimataifa na ulimwengu wa utandawazi. Uuzwaji huo huambatana na mabadiliko ya umiliki wa hisa (*shareholders*), mikataba ya mauzo au miliki na uendeshaji kubadilika au kubakia hivyo hivyo. Aidha, ni suala la kawaida kwa makampuni ya Kimataifa kubadili majina kama mkakati wa kujitana kibiashara kwa upande mmoja (*expansion of market share*) au kutokana na mabadiliko ya mmiliki, kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kubadilisha umiliki wa hisa kwa biashara ile ile, stahiki ya Serikali inategemea Sheria mbalimbali za kodi zilizopo, aina ya mabadiliko ya umiliki wa hisa, mfumo wa umiliki wa hisa kati ya wana hisa wa ndani na nje ya nchi na uandikishwaji wa wanahisa husika (makampuni) ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mifumo miwili iliyotolewa na Mheshimiwa Chiku Abwao kuhusu kubadilisha umiliki kwa biashara ya *Hotel* ya *Sheraton* kuwa *Royal Palm* na baadaye *Movenpick* na sasa *Serena*; na Kampuni ya *Zain* sasa kuitwa *Airtel*; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijapata kodi yoyote kutokana na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano wa *Sheraton*, *Royal Palm*, *Movenpick* na sasa *Serena* kinachobadilika badilika ni mwendeshaji wa hotel na wala siyo mmiliki wa hotel hiyo. Mmiliki wa hoteli ambaye ndiye mlipakodi ni kampuni ambayo haijabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kampuni ya ubia ya *Celtel* kuuzwa kwa *Zain* na kisha *Zain* ikauzwa kwa *Airtel*, Serikali haikupata mapato ya kodi yoyote. Kampuni zilizouzwa siyo za *Celtel Tanzania* na *Zain Tanzania* ambazo Serikali ya Tanzania ilikuwa na hisa huko bali ni *Celtel Africa BV* na *Zain Group of Bahrain* ambazo hazikuwa na uraia wa kikampuni wa Tanzania.

Aidha, Serikali ya Tanzania haikupoteza chochote katika *Celtel Tanzania* na *Zain Tanzania* kwa kuwa imeendelea na umiliki wake wa hisa asilimia 40. Kilichofanyika ni kubadilisha majina tu kutoka *Celtel Tanzania* na kuwa *Zain Tanzania* na hivi karibuni kutoka *Zain Tanzania* na kuwa *Airtel Tanzania*.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa makampuni ya kimataifa yamekuwa yakitumia kiujanja kubadilisha muundo ili kukwepa kodi: Je, Serikali imefikia wapi mpango wa marekebisho wa Sheria za Kodi ili kuendelea kupata stahiki zetu kwa mauzo ya nje?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria tulizonazo zinataka kampuni ikiwa kuna mabadiliko ya wamiliki tuweze kupata *withholding tax*. Ikiwa kuna mabadiliko ya wanahisa tunatakiwa tupate *stamp duty* au ushuru wa stempu na pale ambapo yanahusisha ardhi na majengo tunatakiwa tupate *withholding tax capital gain* na mapato yanayotokana na uwekezaji. Yote haya yanafanyika chini ya Sheria ya Kodi, sura 332 na Ushuru wa Stempu sura 189.

Sasa wakati mwingine siyo tatizo la udhaifu wa Sheria zetu ambao unasababisha tukose mapato, lakini kunakuwa na ujanja ambao pengine unafanywa na wawekezaji. Kukwepa kodi takribani kila mtu hujaribu, lakini mara nyingi inapotokea hivi, kwa umakini wa Taasisi yetu ya *TRA* tunakuwa tunafuatilia na tunagundua. Hata hivyo, tunafuatilia uzoefu wa nchi nyingine na karibuni tutaleta mabadiliko kama ni suala la lazima ili tuweze kupata haki zetu.

NAIBU SPIKA: Maswali madogo mawili ya nyongeza kwenye eneo hili, atafuatia Mheshimiwa Leticia Nyerere lakini kabla ya hapo namwona Mheshimiwa David Kafulila. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Moja ya tatizo kubwa ya Serikali yetu ya Tanzania ni uwezo wake wa kukusanya

kodi na miongoni mwa eneo ambalo tunapoteza mabilioni ya Shilingi ni kwenye kukusanya kodi kutoka kwenye Makampuni ya Simu. Mpaka sasa Serikali yetu haina uhakika wa kiasi cha mapato ambayo makampuni haya yanapata. (Makofi)

Uzoefu wa nchi nyingine kama Kenya wana mitambo ambapo mwisho wa mwezi Serikali inakuwa inafahamu kwamba Kampuni ya Vodacom imepata kiasi gani. Kwa hiyo, wanakwenda kuwadai kwamba kutokana na mapato haya mnatakiwa mtulipe kodi kiasi fulani. Sisi hatuna uhakika huo. Kwa hiyo, naomba Serikali itufahamisha ni lini itatengeneza mfumo wa kuwa na uhakika wa kujua mapato ya Makampuni haya ya Simu ili kujua kiasi sahihi cha kodi ambacho tunapaswa kupata? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tunaweza tukawa tunapoteza mapato kwenye matumizi ya simu. Nakumbuka suala kama hili liliwahi kuzungumzwa hapa na lilijibiwa kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia. Naomba nikumbushe kwamba Wizara hii iliahidi kwamba kuna kifaa ambacho wanakifuatilia ili kifungwe kwenye mitambo ambacho kitatoa data ambazo tunahitaji na zitatupa mapato kamili kutoka kwenye matumizi ya simu. Kwa hiyo, naomba tuwe na subira ili Serikali ifuatilie na kuhakikisha kwamba kifaa hicho kinafungwa na manufaa ya kutumia simu tunayapata.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Hivi Serikali haijaka ikajijuliza ni kwanini Hoteli ibadilishwe majina mara tano ndani ya miaka michache na kwa nini basi hizi hoteli zinabadilishwa kama hakuna sababu ya msingi ambayo itaweza kutupelekea sisi kama Taifa kupoteza pato kubwa kupitia kodi? Naomba sasa Serikali ianze kuwa serious, ifuatilie mabadiliko ya kila leo kwa Mahoteli haya ya wageni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, mko tayari? Kuwa serious sasa? (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, hoteli zinaendeshwa na *management* tofauti ambazo zinajengeka kwenye *chains*. Sasa, hili linatokea kwamba mwenye hoteli anaamua kwamba hoteli yake anapendelea iendeshwe na *chain* gani kwa ajili ya biashara zake lakini hilo halibadilishi umiliki wala halibadilishi mlipakodi. Mwenye hoteli kwa maana ya *owner* ndiye ambaye anatakiwa alipe kodi na ndiye mlipakodi. Kwa hiyo, majina yasiituletee hisia ya kuwa tunapoteza. Naomba niseme kwamba TRA wako makini kufuatilia masuala haya kwa sababu wakati mwingine kuna watu wanaweza wasitoe taarifa zote, wakasema tumebadilisha hiki au kile. Kuna kesi za namna hii ambazo ziko Mahakamani baada ya kufuatilia, na hiyo inawezekana, ikaonyesha kiasi gani Serikali iko serious. Pamoja na hivyo, tutaangalia kama kuna jambo linatupita, tutalifuatilia na tunakubali ushauri wake.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa nipitie kwenye matangazo yetu ya leo. La kwanza linahusiana na wageni walioko katika jukwaa la Mheshimiwa Spika, nao ni wageni wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ambao ni Prof. Santiago Jameniz Barull, Mwenyekiti Mtendaji – MAAT International na Naibu Waziri wa Fedha Mstaafu wa Serikali ya Spain. Pia yuko Dkt. Ruben Pacheko – Mkurugenzi wa Afrika – MAAT international na Balozi Mstaafu wa miaka 28 wa Serikali ya Venezuela. Pia yuko Ndg. Abdul, Ndg. Brayan, Ndg. Dimo – Wakurugenzi wa Afro Center (T) Ltd. (Makofi)

Wageni hawa kwa mujibu wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, wamekuja kwa madhumuni ya kuwekeza hapa Tanzania hasa katika nishati, miundombinu, ujenzi wa nyumba kwa kuanzisha kiwanda chenye teknolojia ya kuweza kujenga nyumba 300 kwa mwezi. Kiwanda cha namna hiyo hivi sasa kiko nchini Angola lakini vilevile wanataka kuangalia mambo mengine. (Makofi)

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 45 kutoka Chuo Kikuu cha Elimu cha Mkwawa kilichopo Iringa wakiongozwa na walimu wao, Ndugu Philemon Sengati na Yusuf Daudi. Wanafunzi wa Mkwawa, ahsanteni sana, tunawakaribisheni sana. Hili ndilo Bunge lenu, tunawatakiwa kila la heri katika masomo yenu. Tunasikitika sana pakitokea migomo. Tunapenda msome na mmalize salama. Ahsanteni sana. (Makofi)

Wanamichezo 40 wa Kikundi cha Kitambi Noma kutoka Zanzibar. Hawa ndugu zetu wa Kitambi Noma kutoka Zanzibar wanaongozwa na ndugu Mohamed Suleiman ambaye pia ni Afisa Tawala Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Mwenyekiti wa Vyama vya Michezo Zanzibar (ZABESA). Mwenyekiti wa Kitambi Noma ni ndugu Suleiman Mohamed. Karibuni sana ndugu zetu kutoka Zanzibar, hili ndilo Bunge lenu, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tuna Maafisa wanne kutoka Shirika la Nyumba la Taifa. Karibuni popote pale mlipo Maafisa wetu. *(Makofi)*

Tuna wachama sita wa Asasi ya *Development Association for Tanzanians* ya Kisarawe – Pwani. Karibuni sana ndugu zangu kutoka Kisarawe. Niwahakikishieni kwamba Mbunge wenu Mheshimiwa Jafu anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Matangazo ya vikao vya kazi za Kamati. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo ya Bunge ya Viwanda na Biashara kwamba kutakuwa na kikao leo kuanzia saa 7.00 mchana. Nadhani niseme kutakuwa na kikao mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge katika ukumbi namba 231.

Mheshimiwa David Silinde, Kaimu Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba leo baada ya kuahirisha Bunge, kutakuwa na kikao cha Wabunge wote wa Chama hicho Bungeni katika ukumbi ambao mmeuzoea.

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, anaomba wajumbe wa Kamati yake ya Fedha na Uchumi kwamba kutakuwa na kikao katika ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya shughuli za hapa kuahirishwa.

Mheshimiwa Diana Chilolo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo kwamba mara baada ya kumaliza kikao hiki, mkutane Pius Msekwa "B".

Waheshimiwa Wabunge, pia mtakumbuka kwamba juzi Ijumaa, tarehe 3, tulifanya maamuzi hapa ya kuomba Kamati yetu ya Huduma za Jamii kwa niaba yetu sote ianze mara moja kazi ya kufuatilia suala zima la mgomo wa Madaktari. Maamuzi hayo yalifanyika tarehe 3 Ijumaa. Tarehe 4 Jumamosi waliondoka kwenda Dar es Salaam na kuanzia jana wameanza kuifanya kazi hiyo na leo na kesho wanaendelea. Kazi hii wanaifanyia katika ofisi za Bunge Dar es Salaam. *(Makofi)*

Niwashukuru sana Madaktari wote ambao wamekubali kukutana na Kamati yetu na wadau wengine wote na niendelee kuwasihii waachane na mgomo ili Watanzania wapate huduma yao muhimu ambayo tunaitegemea kwa kurudi kazini. *(Makofi)*

Kwa kuwajulisha tu Waheshimiwa Wabunge, Kamati yetu kwa leo na kesho itakutana pamoja na watu wengine, wengine imekutana nao jana, lakini kwa leo na kesho itakutana na Katibu Mkuu Utumishi, mnajua kuna mambo ya Utumishi katika suala zima la mgomo wa Madaktari, itakutana na Baraza la Madaktari, itakutana na Baraza la Wafamasia, itakutana na uongozi wa Madaktari wa Mafunzo (uongozi wa Madaktari wanaofanya mafunzo kwa vitendo), watakutana na uongozi wa Jumuiya ile ya Madaktari – MAT, watakutana na Umoja wa Madaktari, watakutana na Kamati ya Madaktari Bingwa, watakutana na Wakurugenzi wa Bodi ya Hospitali ya Muhimbili, watakutana na uongozi wa Vitengo vya MOI, Ocean Road, watakutana na uongozi wa KCMC, watakutana na uongozi wa Bugando, watakutana na uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mbeya, watakutana na Wakuu wa Hospitali za Temeke, Mwananyamala na Amana. Vilevile watakutana na viongozi wa Madaktari mbadala - wale wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Watakutana pia na wadau wengine ambao sijawataja hapa. Nilitaka tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Kamati yetu inapata ushirikiano mzuri sana na inaendelea kufanya kazi ambayo tumeomba wafanye kwa niaba yetu. *(Makofi)*

Kuna tangazo moja la wageni, nilisahau hapa, la Mheshimiwa Tundu Lissu, yeye anaomba kuwatambulisha wajumbe wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Singida Mashariki na uongozi wa CHADEMA wa Wilaya ya Singida Vijijini. Popote pale walipo wasimame. Ahsanteni sana. Ujumbe huu unaongozwa na Mwenyekiti, Ndg. Andrea Andalu. Karibuni sana Bungeni, karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Pia liko tangazo la Mheshimiwa Lucy Owenya, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote na kuwakaribisha Moshi, Kilimanjaro, tarehe 26 Februari, kuna Mbio za Kimataifa za Kilimanjaro Marathon. Anawakaribisheni Waheshimiwa Wabunge kushiriki ili kulinda afya zenu na vilevile ku-support michezo hiyo. Mbio hizi ni za Kimataifa, wanakuja wageni wengi kutoka pande zote za Dunia. Waheshimiwa Wabunge wote tunakaribishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Wabunge wote wa CCM, anawaomba Wabunge wote wa CCM kwamba simu zao ziwe on, mnaweza mkaitwa wakati wowote kwa ajili ya kikao cha CCM, in case ikitokea hivyo lakini kwa sasa bado hajasema chochote. Anaomba tu muwe katika maeneo ambayo mnaweza mkapatikana.

Pia, Kamati yetu ile ya Huduma za Jamii, itakutana na uongozi wa TUGHE na vile vile uongozi wa Chama cha Wauguzi pamoja na wadau wengine.

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu, naomba nitoe pongezi nyingi sana kwa Chama cha Mapinduzi, kwa kufikisha miaka 35 jana. *(Makofi)*

Sasa wengine mbona hawapigi makofi! Jamani, hii ni *birth day party* tu! *(Kicheko/Makofi)*

Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Tunatoa pongezi sisi Wabunge wote kwa Chama cha Mapinduzi kufikisha miaka 35. Ni miaka mingi, si wote wanaweza kufikisha miaka kama hiyo katika uongozi na kwa kweli sherehe zile katika Jiji la Mwanza jana zilisheni kwelikweli, maana Uwanja wa Kirumba ulijaa, ukafurika, ukatapika mpaka nje. Hiyo maana yake ni kwamba tuna-beep, tunaomba njia kwa watani zetu. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mkiona *Order Paper* ya leo, baada ya kipindi hiki cha maswali, tutakuwa tumeishia hapa na sababu yake ni kwamba pamoja na shughuli ambazo zilikuwa zimepangwa hapo kabla kwa tarehe ya leo na Kamati ya Uongozi, lakini kama mnavyojua Kanuni ile ya 85(1) ambayo inasema "Kamati iliyopelekewa Muswada na Spika, itakapokamilisha kujadili Muswada huo, Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Spika kwa maandishi kwamba Kamati imemaliza kujadili Muswada husika". Bado kidogo jambo hili halijakamilika kwa hatua zake zote katika ngazi ya Kamati, kwa hiyo hatuwezi kushughulika nalo leo. Hii inafuta maelezo yale yote ya kusema unajua, unajua, hayo ndiyo maelezo yake.

Waheshimiwa Wabunge, sasa shughuli zangu hapa Mezani zimekamilika na kwa kuwa sasa *Order Paper* yetu imekamilika...

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Basi, naomba wale wote ambao mnataka kuomba Mwongozo msimame niwape nafasi kwa mpigo. Ni watatu eeh? Ngoja niwaandike! Naona ni watatu. Basi, tuanze mlivyojipanga, moja, mbili, tatu!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kutoa hoja kwamba tujadili jambo la dharura lililoulizwa na Mheshimiwa Machali wiki iliyopita kuhusu Maaskari walioua watu kule Kasulu, sasa Maaskari wale wameletwa Jimboni kwangu Kibondo ili waendeleze mauaji. Sasa naomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ili tuweze kujadili suala hili kwa sababu muda upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Haya, anayefuata!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kwa kunipa fursa hii ili niweze kuzungumzia jambo moja.

Nasimama hapa kuweza kuomba Mwongozo juu ya jambo lililotokea siku ya Ijumaa wakati Mwenyekiti, Mheshimiwa Mabumba akiliahirisha Bunge. Bunge lilikaa kama Kamati wakati tunajadili kuhusiana na *issue* ya *Anti-Money Laundering*. Tulipokaa kama Kamati, tulifanya maamuzi, baada ya

kufanya maamuzi, Mheshimiwa Ole-Sendeka alisimama na kuomba Mwongozo wa Kiti cha Spika. Sasa maamuzi yalishafanywa na Kamati kwa mujibu wa hii *schedule of amendment* juu ya adhabu kutoka kwenye miaka mitatu, kutokana na *issue* ile ambayo tulikuwa tunajadili ya *Anti-Money Laundering*. Sasa maamuzi yaliyofanywa na Bunge likiwa limekaa kama Kamati, yalikuja kubatilishwa na Kiti peke yake pasipokutuhaji Waheshimiwa Wabunge na wakati tumeshafanya maamuzi.

Binafsi nimekaa na kutafakari sana hasa ukienda kwenye Kanuni ile ya 79 juu ya uamuzi wa Bunge, naona kama Kiti kilikiuka utaratibu. Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako juu ya hali hiyo kwa sababu siyo jambo la kawaida, Bunge limekaa, limeamua, halafu Spika akafanya vinginevyo. Naomba Mwongozo wako, ni kwa nini hali hiyo ilijitokeza, naona kama vile kuna ukiukaji wa taratibu katika suala zima la utungaji wa Sheria, Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Sasa ni Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika...

KUHUSU UTARATIBU

MBUNGE FULANI: Kuhusu Utaratibu!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mnyika malizia, halafu tutaendelea.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Naomba Mwongozo wako kwa jambo hilihilo lakini kwa kurejea Kanuni ya 88(8) ambayo inasema kwamba:-

"Baada ya mtoa hoja kuhitimisha hoja yake ya mabadiliko, Spika atalihoji Bunge ili kupata uamuzi kuhusu hoja hiyo ya mabadiliko".

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kanuni ya 89(1) ambayo inahusu Miswada kusomwa Bungeni kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ule wa Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu (*Anti-Money Laundering Amendment Act*), ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Pili na kupitishwa kwa Mara ya Pili. Naomba Mwongozo wako vilevile kwa mujibu wa Kanuni ya 91 ambayo inasema kwamba:-

"Baada ya Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Tatu, utahesabika kuwa umepitishwa na Bunge".

Sasa, katika jambo hili, Ibara ya 19 ambayo ilikuwa ina mapendekezo ya marekebisho ya kwangu na ya Mheshimiwa Mkosamali kuhusiana na kuongeza adhabu kwa wanaobainika kukutwa na makosa ya fedha haramu, kilipitishwa na Bunge, kwa sababu hiyo, kilipitishwa kwenye Kamati. Kilipitishwa Muswada uliposomwa Mara ya Pili vilevile kilipitishwa Muswada uliposomwa Mara ya Tatu. Itakuwa kinyume kabisa na mamlaka na hadhi ya Bunge kwa mujibu wa Katiba ya nchi Ibara ya 63(3) kama maamuzi yale yaliyofanywa na Bunge yakafutwa tu kwa kauli ya Mwenyekiti ya mwishoni mwa mkutano ya kutamka kwamba, "nimefuta maneno yangu pamoja na marekebisho yake". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ili maamuzi halali ya Bunge yabaki kuwa maamuzi ya Bunge. *(Makofi)*

KUHUSU UTARATIBU

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuomba Kuhusu Utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 53(8) pamoja na Kanuni ya 5(4). Kanuni ya 53(8) inasema:-

"Mbunge yeyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo lilikwishakuamuliwa ama katika mkutano huo uliopo au ule uliotangulia, wala kuwahisha...)"

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Kanuni ya 5(4) inasema:-

"Mbunge yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza kuwasilisha sababu za kutoridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika".

T A A R I F A

MBUNGE FULANI: Taarifa!

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kueleza hayo kwa sababu ninatambua vifungu ambavyo Waheshimiwa wote wawili Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Machali ambao wameeleza na ninakubaliana nayo hayo, lakini kwa mujibu wa hiyo Kanuni ya 53(8), kuna tofauti kati ya Mkutano na kikao. Huu ni Mkutano wa Sita lakini Kikao cha Tano, Kikao cha Nne kilifanyika siku ya Ijumaa kwa maana ya taratibu za Kanuni hii, Mkutano huo ulikwishapita kwa hiyo jambo hili lisingeweza kurejeshwa na mtu akitaka kurejesha inabidi afuate utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna mkanganyiko katika suala la maamuzi hayo kwa mujibu wa maelezo ya Wabunge, nakuomba ili jambo hili liweze kutendewa haki, mwenye nia jambo hili liweze kurekebisha afuate utaratibu huo au angekuomba wewe ulielekeze jambo hili kwenye Kamati ya Kanuni kama ambavyo Kanuni ya 68 inavyokupa wewe mamlaka ya kulielekeza jambo hilo kwenye Kamati yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa hiyo ya utaratibu ili tusije tukajichanganya na hasa ukizingatia kwamba kulikuwa tayari na uamuzi wa Spika siku ile kuhusu jambo hili.

T A A R I F A

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

NAIBU SPIKA: Mbona hamnipi nafasi? Tulieni kwanza, Mheshimiwa AG kwanza.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu linatawaliwa na Kanuni, ni kweli kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 91 uamuzi ukishafanyika umefanyika lakini vilevile kama uamuzi uliofanyika ulikuwa wa makosa na kama Bunge limepitisha Muswada ambao baadaye unaonekana kuna makosa katika kikao hicho, kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Cap.1, *Interpretation of Laws Act*, kifungu cha 24, kinaruhusu Bunge hili kufanya mabadiliko katika kikao hichohicho kimoja.

Pili, kwenye Kanuni, Wabunge wameshakuwa maarufu kwenye Kanuni lakini zile ambazo haziwaungi mkono huwa hawazipitii. Kanuni ya 54(4) inaweka *exception* inasema:-

"Hoja ambayo, kwa maoni ya Spika ina lengo la kutaka jambo ambalo lilikwishaamuliwa na Bunge katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kabla ya kikao kinachoendelea ifikiriwe tena, haitakubaliwa na Spika, isipokuwa tu kama ni hoja ya kutaka uamuzi wa Bunge uliokwishafanyika ubadilishwe".

Kwa kuzingatia hayo, Serikali ilikuwa imepanga kuwasilisha kwako taarifa ya kutoa hoja ili kusudi Bunge lako likikaa kama Kamati ya Bunge Zima lifanye maamuzi kuamua hoja ambayo sisi tutatoa hapa. Ni kweli kwamba kwa utaratibu ule wa Kanuni ya 91 huwezi kusahihisha kosa lililofanyika nje ya ile Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa mujibu ya Kanuni ya 54(4), ninatarajia kuwasilisha hoja kwenye Bunge lako Tukufu ili kusudi tufanye maamuzi, tusahihishe yale makosa yaliyofanyika siku ya Ijumaa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu uwe wa mwisho katika jambo hili.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kinachozungumzwa na hizi Kanuni, Kanuni ya 54(4) ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameinukuu ni kubadilisha maamuzi ya Bunge. Kilichobadilishwa na wanachokigombea Wabunge, Mheshimiwa Machali pamoja na Mheshimiwa Mnyika ni kwamba Bunge lilishafanya maamuzi, halafu Mwenyekiti, bila kuzingatia Kanuni akabadilisha maamuzi

ya Bunge wakati hana mamlaka. Kwa hiyo, hapa kinachohitaji kubadilishwa au kurekebisha siyo uamuzi wa Bunge ni uamuzi wa Mwenyekiti aliye-act irregularly and illegally. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Hapa ipo shughuli, maana kuna mambo mawili hapa siyo moja. Tunafuatilia huu mjadala eeh, hapa yapo mambo mawili.

Kabla ya hapo, tuanze na suala la Mheshimiwa Mkosamali ambaye ndiye alianza na kutaka suala la dharura liingie tujadili suala la Maaskari wanaodaiwa kuua watu huko Kasulu na amefanya hayo kwa kutumia Kanuni ya 49(1). Sasa namwomba Mheshimiwa Mkosamali hebu atusomee hiyo Kanuni ya 49(1). (Kicheko)

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu likubali kwamba uliniinua kwa ghafla sana, ni Kanuni ya 47(1). (Kicheko)

NAIBU SPIKA: Tusomee tu Kanuni ya 49(1) kwanza inasemaje?

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika ni Kanuni 47(1) ndiyo ambayo nilikuwa ninanukuu. (Kicheko)

NAIBU SPIKA: Basi bwana, yeye Kanuni aliyoitumia ni 49(1) ambayo ni Waziri anaweza kutoa Kauli Bungeni kuhusu jambo lolote linalohusu Serikali. Kwa hiyo, bahati mbaya, wakati mwingine utakumbuka kuwa sahihi zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, tukimaliza hilo tunakuja kwenye suala zima hili ambalo limetuchukulia muda wa kutosha hapa, niseme tu kwamba ni sahihi kwa wale wote waliofanya nukuu katika Kanuni yetu ya 91 maana inasema kabisa kwamba baada ya Muswada Kusomwa Mara ya Tatu utahesabika kuwa umepitishwa na Bunge. Kwa hiyo, sasa haya yote yaliyotokea na yanayoendelea, kwa kweli yanahitaji tafakuri makini. Kwa hiyo, mimi naomba mtupe nafasi ya kulitazama jambo hili, tumepata ushauri wa Serikali wa namna ya kuenenda nalo, tumesikia na upande wenu na kwa jinsi hiyo basi ninaiomba Kamati ya Kanuni iweze kukutana haraka sana iwezekanavyo ili kuweza kumshauri Spika namna bora zaidi ya kuliweka vizuri jambo hili kwa sababu ni jambo la kikanuni.

Waheshimiwa Wabunge baada ya maelezo hayo kama nilivyosema, kwa siku ya leo, shughuli zetu zimekamilika kwa hiyo nahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Jumanne tarehe 7 Februari, 2012, saa Tatu kamili asubuhi. (Makofi)

*(Saa 5.30 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,
Tarehe 7 Februari, 2012, saa tatu asubuhi)*